**IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH**

**(ISSN: 2805-413X)** ***Dkt.Aggrey Wanyama, ****

https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*

*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

# Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.

Dkt.Aggrey Wanyama, Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta

Dkt.Rose Kawira, Chuo Kikuu cha Mount Kenya

Mary Nyambura Mwangi, Chuo Kikuu cha Mount Kenya

**Ikisiri**

*Kila mwandishi huathiriwa na sababu mbalimbali katika usawiri wa wahusika kwenye utunzi wake. Ni kwa sababu hii basi tumeweza kuchunguza athari ya jinsia ya mwandishi katika usawiri wa wahusika katika riwaya za Kiswahili. Tumeweza kubainisha jinsi usawiri wa wahusika katika riwaya huathiriwa na jinsia ya mwandishi. Hii ni kwa sababu kuwa wahusika katika riwaya huwa wengi na husawiriwa kwa njia mbalimbali. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza athari ya jinsia ya mwandishi katika usawiri wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Lengo hili lilitimizwa kupitia kwa lengo mahususi ambalo ni; kutathmini athari ya jinsia ya mwandishi katika usawiri wa wahusika kwa njia chanya au hasi ili kuwakweza au kuwatweza. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Ufeministi wa Kiafrka iliyoasisiwa na Steady (1981). Utafiti huu ulifanyika maktabani. Data ilikusanywa kupitia usampulishaji lengwa kutoka katika riwaya teule ambazo ni Nyuso za Mwanamke (2010) Said A Mohamed na Nguu za Jadi(2022) Clara Momanyi. Data hii imechanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa mujibu wa malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Utafiti huu utawafaidi wasomi, watafiti na wahakiki wa kazi za kifasihi kwa kuwa utachangia kujaza mapengo katika utafiti hasa kuhusu masuala ya kijinsia. Vilevile, tumekusudia utafiti huu uweze kuwafaidi wahakiki na wasomi katika kuzitafiti kazi nyinginezo za kifasihi. Mbali na hayo, utafiti wetu utatumika kama katika marejeleo kwa watafiti wa masuala ya kijinsia wa siku zijazo katika uendelezaji tafiti zao.*

**Dhana Muhimu**

**Chanya, Hasi, Jinsia, Kweza, Tweza, Usawiri, Ubabedume, Wahusika**

## Utangulizi

Wahusika ni nyenzo muhimu katika kufanikisha uhalisia wa kazi ya msanii au mwandishi katika utanzu husika. Waandishi huwachora wahusika wao kwa lengo la kuwasilisha maudhui ya kazi zao kwa jamii husika.Wahusika ndio kisemeo muhimu cha msanii wa kazi ya fasihi. Jinsi watunzi wanavyowasawiri wahusika hawa kwa njia moja ama nyingine huwa ni kutokana na athari ya jinsia yao binafsi kuwaelekea wahusika wa jinsia mbalimbali katika tungo zao. Chesaina (1987) alichunguza jukumu na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa, na Kiswahili. Alisoma waandishi wa kike na wa kiume na kuonyesha kwamba waandishi wa kike wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika jinsi wanavyowasawiri wahusika wa kike. Hoja yake kuu ni kwamba wanaume wanapokuwa wanandika kuhusu masuala ya kike, wanakumbana na vikwazo kwa sababu wao wenyewe hawajakumbana na dhuluma hizi binafsi na hivyo hawawezi kuelewa kwa undani hali ya mwanamke. Lugano (1989) ameangazia usawiri wa mwanamke katika riwaya nne za Euphraise Kezilahabi. Kwa mujibu wa Lugano, Kezilahabi ni mwandishi wa kiume anayekatisha tamaa juhudi za ukombozi wa mwanamke, kwani anaendeleza falsafa ya jamii yake kuhusu mwanamke, ambayo inamchukulia mwanamke kama kiumbe duni chini ya utawala wa mwanaume.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X)
https://ijojournals.com/
Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
Dkt.Aggrey Wanyama, *


Katika makala hii, tunaangaziausawiri wahusika wa jinsia mbalimbali kwa njia chanya na hasi katika riwaya za Kiswahili kama kiwakilishi cha athari ya jinsia ya mtunzi katika usawiri wa wahusika hawa.

**Mwandishi alivyomsawiri mwanamke katika Riwaya ya *Nguu za Jadi* (2021) kwa upande chanya.**

**Mwanamke kama mtu wa Kujitegemea**

Mwanamke amechorwa kama kiumbe wa kujitegemea. Mangwasha anaalisi kuwa ni ada ya binadamu kufanya kazi ili aweze kulisukuma gurudumu la maisha. Hii inadhihirika hivi:

*Ni ada ya binadamu kufanya kazi ili aweze kulisukuma gurudumu la maisha. Ni adhaa kuwategemea wengine kukuendeshea maisha. Haijalishi hata kama ingemlazimu kutumia sauti yake kuwatumbuiza au kuwachekesha watu katika kumbi za tafrija. Au kutumia mikono yake kupasua mawe na kokoto. Kazi ni kazi, bora imhakikishie tonge mwishoni mwa siku. Aliamini kwamba hata kama angepigwa kalamu, kamwe wanawe hawangelala njaa. (uk.12)*

Mwanamke mara nyingi amechorwa kuwa kiumbe asiyeweza kujitegemea kwa hali yoyote ile,hili mara nyingi humfanya mtumwa wa mwanaume katika asasi nyingi za kijamii.Hivyo basi,mwanamke anayejitolea kufanya kazi kwa bidii na kuweza kupata kipato chake huwa anapunguza jambo hili la kuonekana mtumwa kwa mumewe na hivyo kwa kufanya hivi anaweza kumiliki uhuru wake kama mwanaume katika jamii.Hili linaunga mkono maoni yake Ogundipe-Lleslie (1994), anayesema kuwa mwanamke ndiye anayefaa kufahamu kuwa yeye ndiye ana uwezo kufafanua uhuru wake na kuelewa kile hasa anachokihitaji.

Kulingana na Steady (1981), Ufeministi wa Kiafrika unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika, unatarajiwa kuchunguza hali ya kijamii na kitamaduni zinazochangia unyanyaswaji wa wanawake wa Kiafrika.Anaendelea kudai kwamba, mwanamke wa Kiafrika ni mtetezi wa haki na usawa wa wanawake kuliko mwanamke wa Kimagharibi kwa kueleza hivi:

*Ufeministi wa kweli ni ile hali ya kujinyima ulinzi wa kiume na jitihada za kuwa na busara na uwezo wa kujitegemea.* (uk.21-34)

Ndoa imetokea kuwa asasi ambayo mwanamke huwa anagandamizwa zaidi, humfanya mwanamke kupoteza uhuru wake kwanza ikiwa mwanamke hana mbinu mbadala ya kuvumbua riziki na hivyo kumfanya kuwa mtegemezi wa mwanamume. Millet (1977) anasema kuwa:

*Asasi kuu inayoendeleza ubabedume ni ndoa. Ndoa hupelekea kuwepo kwa familia. Familia ni kitengo muhimu katika kuimarika kwa ubabedume kwa kuwa viongozi wa familia hizo ni wanaume.*

Wamitila (2002:157) anasema kuwa ndoa ni asasi mojawpo ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizwaji wa wanawake. Asasi yenyewe imejengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanaume na kuishia kumwangalia mwanamke kama chombo.

Mangwasha anaonekana kuukabili utegemezi huu kwa kujituma katika kazi pale ofisini kwa Chifu Mshabaha.Ana uwezo wa kukidhi mahitaji yake pamoja na ya watoto wake na hivyo kutokuwa mtegemezi kwa mume wake Mrima ambaye ni mlevi wa kupindukia.

**Mwanamke kama mpenda elimu**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Elimu ni kitu muhimu katika maisha ya binadamu yeyote yule kwani kupitia kwa elimu binadamu huweza kupata utambuzi wa masuala mengi ya kijamii. Millet (1969) anasema "Kama elimu ni nguvu, nguvu pia ni elimu" Mwanamke wa Kiafrika mara nyingi hunyimwa fursa ya kupokea elimu ama elimu anayopokea huwa ni duni na ambayo haiwezi kumsaidia. Sababu ya kimsingi ya kumnyimwa mwanamke huyu elimu huwa ni kumfanya kuwa mjinga na hivyo kumtawala kwa njia iliyo rahisi na hivyo kufaulisha mfumo wa ubabedume.

Hata hivyo mwanamke katika riwaya hii amechorwa kama mhusika anayependa elimu na kutaka kuiendeleza. Tunaelezwa na mwandishi kuwa Mangwasha licha ya kutopata alama ya kujiunga na Chuo Kikuu anamshauri babake Mzee Shauri kumpeleka katika Chuo cha Uhazili kwao Ndengoni.Pale anahitimu na kuajiriwa katika afisi ya Chifu Mshabaha. Mwandishi anaeleza:

*Mangwasha alijulikana kama mwenye bidii na ari kubwa ya maendeleo. Masomo yake yalifika ukingoni alipomaliza kidato cha nne. Hata hivyo, bado alikuwa na hamasa kubwa ya kuendelea na masomo. Kwa hivyo, alifaulu kumshawishi baba yake, Mzee Shauri, ampe ruhusa ya kuendelea na masomo. Ijapokuwa hakupata alama zilizomwezesha kujiunga na chuo kikuu, alijiunga na chuo cha uhazili kwao Ndengoni.Alihitimu na kuajiriwa mjini Taria katika afisi ya Chifu Mshabaha. (uk.14)*

Mwangwasha anafahamu kuwa ni elimu pekee inayoweza kumkombolewa hadhi katika jamii yake yenye mfumo wa kuumeni na hivyo ang`ang`ania baba yake kumpeleka shule ili kutimiza ndoto zake. Japo ana ufahamu kuwa matokeo yake ya kidato cha nne hayakuridhisha ila hakati tamaa. Na hivyo kutokana jitihada zake anafuzu na kupata kazi katika afisi yake Chifu Mshabaha.Kazi hii inampa nguvu za kiuchumi ambazo ni mwanaume huwa nazo katika jamii ya Kiafrika.

**Mwanamke kama mwajibikaji**

Mhusika mwanamke amesawiriwa kuwa mwajibikaji kazini na mwandishi. Amedhihirishwa kama mhusika hodari aliyefika kazini mapema, kaondoka wa mwisho, akawa na mlahaka mzuri na watu. Anasema hivi:

Alikuwa msichana hodari sana katika kazi, akapendwa na watu aliowatumikia. Alikuwa wa kwanza kufika afisini lakini wa mwisho kuondoka. Aliwatumikia watu kwa moyo mkunjufu. Hakuna aliyefika afisini mwake akatoka na manung`uniko. Huduma zake zilisifika kote mjini Taria.Utiifu na umahiri wake vilimwezesha kupandishwa cheo hadi kufikia gredi ya juu kabisa ya uhazili.

Vilevile hili linadhihirika wakati Mangwasha analazimika kujitwika jukumu la kuwalea wanawe baada ya mumewe Mrima kuzama katika ulevi. Mwandishi anaeleza kuwa:

*Mangwasha alimsimulia Mbungulu yote yanayomsibu. Alimweleza jinsi anavyojitwika jukumu la kuwasomesha, kuwalisha na kuwavisha watoto wao pekee yake. Ile jadi ya mwanamume kuwa kichwa cha nyumba sasa haipo tena. Mangwasha keshaivunja jadi hiyo bila kutarajia wala kunuia. Mrima haonekani kujitwika majukumu yake ya unyumba tena. Anakesha na kuamkia ulevini. Hana habari tena kuhusu familia yake. Haya yalimchosha Mangwasha.Wala hakudhani Mrima angebadilika kiasi hicho. (uk.17)*

Kwa karne nyingi mwanamke amesawiriwa na jamii yake kuwa mtegemezi wa mwanaume kwa takribani kila kitu. Lakini namna siku zinavyosonga na mtoto wa kike kupata elimu inayompa uwezo wa kiuchumi wa kutekeleza baadhi ya masuala hata kama si yote, mtazamo

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

huu hasi unaendelea kupoteza nafasi yake katika jamii ya Kiafrika.Mangwasha anamweleza rafiki yake Mbungulu kuwa imemlazimu kujitwika jukumu la kuwalea watoto wake kwa kuwasomesha, kuwalisha na kuwavisha pekee yake licha ya kuwa na mwanamume aliyemwoa ambaye amekuwa akikesha ulevini na kuamkia huko vilevile.Kulingana na Mangwasha ile jadi ya mwanaume kuwa kichwa cha nyumba inaendelea kutoweka kwa sababu yale aliyokuwa akiyatekeleza mwanaume kwa sasa mwanamke ana uwezo wa kuyatekeleza mara dufu.

**Mwanamke kama mlezi mwema katika jamii**

Mwanamke amechorwa vilevile kuwa ndiye mlezi wa familia. Baada ya Mrima kujitosa katika ulevi na anasa, jukumu zima la ulezi wa watoto linakuwa la Mangwasha.Anaamua kutafuta mumewe aliyepotelea katika ulevi. Anasaidiwa na rafikiye Mbungulu kumtafuta Mrima katika nyumba za uuzaji pombe. Mwandishi anatueleza hivi:

*“Baba Sayore, nina maneno machache ya kuongea nawe”, Mangwasha alianza.*

*“Ha! Tangu lini mwanamke akawa na machache. Mna maneno mengi kama chiriku”, Mrima alitamka kwa kejeli.*

*“Ninaomba kujua jana ulikuwa wapi hadi kunijia alfajiri”,*

*Mangwasha aliuliza taratibu bila kuonyesha kuchukizwa.*

*“Koma…koma hapo! Tangu lini mke amuulize mumewe kule aendako au atokako? Hivyo ndivyo ulivyofunzwa na mamako? Ama kweli, wananwake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee”, Mrima alilipuka.*

*Sikiliza, Mrima, mume wangu. Hukunikuta msungo uliponioa. Nilifunzwa ada zote za mila zetu. Hata hivyo, sikuambiwa nisiulize pale panapoharibika. Sikuambiwa niwe tutwe lisilojua kinacholipitikia mbele ya macho yake,” Mangwasha akaja juu.*

*“Ushasikia hata siku moja ngamia kamea pembe? Au shingo ikapita kichwa?”*

*“Mume wangu mpenzi, hata hicho kichwa kispotulia juu ya shingo, kila mara huku na huko, shingo itachoka pia.” (uk.8)*

Suala la malezi ya watoto katika jamii nyingi za Kiafrika limeachiwa mwanamke. Anafaa kulitekeleza hili pasi na kulalamika. Mwanaume huwa hausishwi katika hili ana uwezo wa kuondoka na kuingia nyumbani bila kuulizwa kwani kulingana na itikadi ya jamii hizi mwanamume ndiye kichwa na hivyo hapaswi kuhojiwa kwa kile akitekelezacho. De Beauvoir (1985) anasema:

*Asasi ya ndoa imempa mwanamke majukumu mawili muhimu. Kwanza, ni kuzaa watoto na pili ni kuhakikisha kuwa anatimiza mahitaji ya kimapenzi kwa mumewe na kuangalia nyumba yake.*

Hivyo basi kwa maoni ya De Beauvoir mwanamke wa Kiafrika ana majukumu mawili ambayo ni kuzaa na kumstarehesha mwanaume kimapenzi pindi anapohitaji. Hivi kwamba jambo hili humfanya mwanamke kutazamwa kama chombo tu ambacho haja kuu kwa mwanamume ni kumtumikia. Huu ni utwezaji wa mwanamke kwa njia yoyote ile. Mbona asipewe hadhi anayofaa kama mwanajamii yeyote yule mbali na jukumu lake katika jamii

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*


kuzingatiwa na mhimili wa jinsia yake? Haya ndio bahati ya maswali Wanaufeministi wa Kiafrika huwa wanajiuliza bila kupata majibu na kuishia kuwahamasisha wanawake wa Kiafrika kuwa pindi wafahamupo kuwa ni watumwa wa mwanamume ndipo wataweza kuvumbua mbinu za kupambana ili kujipatia uhuru kutoka kwa mwanamume ambaye amewekwa juu yao. Kutokana na ulevi wake Mrima anapotelea kwa mama nitilie pasi na kujali mahitaji ya watoto wake jinsi yanavyotoshelezwa. Anarejea nyumbani anavyotaka ila hataki kuulizwa na mkewe Mangwasha.

**Mwanamke kama mwenye bidii**

Mwandishi amemchora mwanamke kuwa mtu mwenye bidii. Mangwasha alifahamu kuwa ufanisi wowote ule maishani unatokana na bidii. Alijibidiisha kazini, alijua kuwa hakuna ndoto itakayotimia bila kujishughulisha. Tunaelezwa na mwandishi kuwa:

*Mangwasha hakutaka kuwa mmoja wa watu kama hao. Hivyo, akatia bidi kazini, akawa na tumaini. Alijua kwamba hakuna ndoto itakayotimia bila kujishughulisha. Wazazi wake daima walimkumbusha kuwa uzembe ni likizo ya wajinga. Johari za hekima alizopokea kutoka kwa wazazi zilimshajiisha, akatazamia kesho yenye heri. Aidha, alijua kwamba mwomba Mungu hachoki Akaamini kuwa siku moja nyota yake ingeng`aa maishani. (uk.40)*

Ufanisis wowote wa mwanadamu mara nyingi hutegemea bidii zake takrbani katika shughuli anazozitekeleza kila uchao. Kila mzazi anajukumu la kupanda mbegu hii kwa watoto wake. Mangwasha alifahamu kuwa ufanisi wake ungetokana na bidii zake na hivyo alijukumika katika kazi zake jinsi alivyokuwa ameelekezwa na wazazi wake.

**Mwanamke kama mwenye kusamehe**

Mwanamke amesawiriwa vilevile kuwa mtu ambaye ni mwepesi wa kusamehe licha ya makuruhu yote anayotendewa na mwanamume katika jamii na kumkaribisha. Mangwasha anamsamehe mumewe licha ya kumpitishia magumu kwa kumuacha na wanawe. Mwandishi analidokeza hivi:

*Alipopata nafuu, Mrima alikataa abadan katan kwenda nyumbani kwake. Angeiambia jamaa yake alikuwa wapi siku hizi zote? Alitahayari mno. Ingawa Mangwasha alitamani mumewe kurejea nyumbani, Mrima alikuwa na tatizo. "Hamwoni kwamba mila hairuhusu mie nikatunzwe na mke kama mgonjwa? Au mmeshasahu mikatale ya utamaduni kwa sababu mnaishi mjini?" Mrima aliwauliza akina Lonare walipokuja kumchukua kutoka hospitalini. "Mila zipi hizo? Mume wangu, nani asiyejua uliyopitia?" (uk.100)*

Mara nyingi huwa ni vigumu kwa mwanadamu kumsamehe mwenzake ila msamaha ndio suluhisho ya mengi ya matatizo yanayomsibu mwanadamu katika maisha anayoishi kila siku.Mangwasha anajipata katika njia panda,japo mume wake ambaye amekuwa akiyatelekeza majukumu yake kwa kunywa pombe na hata kutojali wanachokila wanawe,Mangwasha anafikia uamuzi wa kumtafuta mume huyo na hata kumsamehe na kumrai kurejea nyumbani ili wasaidiane katika malezi ya watoto wao.Kwa upande wake Mrima kurejea kwake kwa Mangwasha kungemvunjia hadhi kwa kuwa utamaduni wa jamii yake haukubali mwanamume kulishwa na mwanamke au kuwa chini ya mwanamke.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

**Mwanamke kama mwenye mapenzi ya dhati**

Mwandishi anamsawiri mwanamke pia kuwa ni mhusika mwenye mapenzi ya dhati. Mangwasha alimlisha mumewe na kumvisha licha ya shinikizo la kumuacha kutoka kwa watu kama Sagilu. Hili linadhihirishwa na mwandishi hiiv:

*"Mshabaha yupo au katoka?" Sagilu aliuliza, bila salamu.*

*"Yupo.Pita ndani," Mangwasha alimjibu.*

*"Mbona hujawahi kuniuliza hata siku moja kama ninaweza kumtafutia Mrima kazi serikalini? Au hujatosheka kulisha na kuvisha mtu asiye na be wala te?" Sagilu aliuliza kwa bezo.*

*Mangwasha hakumtazama wala kumjibu.*

*"Hutaki kujibu swali muhimu hivi?"*

*Mangwasha alimtupia jicho akamwambia, Kwa taarifa yako, mume wangu Mrima hahitaji kazi serikalini. (uk.102)*

Kwa kawaida mwanaume ndiye mtunzaji mkuu wa familia katika jamii. Hufaa kuipa familia mahitaji kama vile chakula, mavazi na hata upendo.Endapo mwanamume atashindwa kutekeleza haya na nafasi hii kuchukuliwa na mwanamke jambo hili huchukuliwa kuwa ni mwiko sanasana katika jamii zenye ubabe dume mwingi.Kwa sababu ya mapenzi alinayo Mangwasha anatekeleza wajibu wa mumewe Mrima licha kuwepo na vishawishi vingi vya kumwacha kutoka kwa baadhi ya wanajamii kama vile Sagilu.Sagilu alikuwa na mpango wa kuhakikisha ndoa kati ya Mangwasha na Mrima imesambaratike ndio aipate fursa ya kumteka Mangwasha kimapenzi na kuweza kuzima uchu wake.Sagilu alikuwa mhusika mwenye tabia ya kuwatumikia wanawake kwa ajili ya kuzima kiu yake ya ukware.Wakati anapomweleza Mangwasha kuwa mumewe ameshindwa kutekeleza wajibu wake,ilikuwa ni kishawishi chake kumfanya Mangwasha kumwacha Mrima jambo ambalo Mangwasha anakataa kuliridhia kwa sababu ya upendo wa kweli aliokuwa nao kwa mumewe Mrima.

**Mwanamke kama aliyejikomboa kimawazo**

Mangwasha amejikomboa kmawazo dhidi ya utamaduni unaomdunisha na kumdhalilisha mwanamke. Anapinga kauli za Mbungulu kwamba azingatie yale aliyofunzwa na kungwi na kwamba asithubutu kumfuata mumewe katikza starehe zake. Anaona hizi ni mila zilizopitwa na wakati. Mbungulu anasema hivi:

*"Hapo umetoa kauli za hekima na busara mwenzangu. Sasa umekumbuka aliyokuusia kungwi kwamba ushikilie hekima na busara, na neema uvae shingoni mwako" (uk.39)*

Mwanamke wa Kiafrika huwa anaandaliwa akiwa mdogo jinsi ya kuishi na mwanaume pindi anapoolewa. Huwa anashauriwa kutojiingiza katika masuala ya mwanaume hata kama yale anayoyatenda mwanaume huyu hayafai kamwe. Mrima mumewe Mangwasha anajihusisha na ulevi hivi kwamba suala la malezi ya watoto wake analipuuzilia mbali. Mangwasha anapolemewa na mzigo wa malezi ya watoto hawa anafikia uamuzi wa kuenda kumtafuta Mrima jambo ambalo Mbungulu analipinga kwa kumshauri Mangwasha kukumbuka yale aliyofunzwa na kungwi kuwa hafai kumfuata mumewe katika starehe zake. Mangwasha anapuuzilia mbali maoni haya kwa kuyaona kuwa ni ya kibuzi na yaliyopitwa na wakati na yanatumiwa kumnyamazisha mwanamke.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

**Mwanamke kama mzalendo**

Uzalendo ni ile hali ya kuipenda nchi yako. Mangwasha anaonyesha uzalendo pale anapotamani kukutana na viongozi wa Matuo ili amani iweze kudumishwa nchini. Anajalii sana mustakabali wan chi ya Matuo hasa pale anapowaona watoto na vijana wakiteseka bila matunzo mema ya wazazi wao hata ajira. Uzalendo wake unaonekana pale anapoungana na wanawake wengine kufanya kampeni ili Lonare achukue hatamu za uongozi na kubadilisha hali ya uchumi wa nchi.Mangwasha vilevile anamkabili Chifu Mshabaha kwa sababu ya mawazo yake ya kikabila.Chifu huyu anamtaka mtemi Lesulia kuendelea kuiongoza nchi ya Matuo kwa sababu anatoka katika kabila lake.Licha ya kubainika wazi kuwa mtemi huyu alikuwa akiongoza nchi vibaya kwani kulikuwa na ufisadi wa aina yake,mauaji ya kiholela ya raia.Mangwasha anasema hivi:

*"Naam.Tutahakikisha tumezibomoa hizo hisia zenu za ukabila, ubinafsi na chuki katika nyoyo zenu kabisa!" … "Mnacheza na serikali nyinyi!" Chifu Mshabaha alitamka na kusonya.*

*"Ebo! Serikali unayosema ni nani hasa? Serikali ni sisi wananchi, kaka. Hata huyo Lesulia unajuaje atakuwa mtemi wetu tena? Umeishi ndani ya kivuli cha Lesulia kiasi cha kwamba hujui uchaguzi unabisha? Umo ndotoni wewe! Aliye juu, msubiri chini, kaka. (uk.136)*

Viongozi wengi katika mataifa ya Kiafrika hupata uongozi wao kwa kutumia misingi ya kikabila. Na hutaka kutumia misingi hii kusalia mamlakani licha ya kubainika wazi kuwa sera zao za kiutawala ni hasi na hazina natija kwa raia wake. Chifu Mshabaha anaonekanaa kulifumbia jicho hili na kuutetea uongozi wake mtemi Lesulia.Anaiona serikali ya mtemi Lesulia kuwa ni yao kwa sababu Lesulia ni wa kabila lao. Mangwasha anamkumbusha Chifu Mshabaha kuliondoa hili katika mawazo yake kwani uchaguzi umekaribia na serikali wanayodai kuwa ni yao itaondolewa mamlakani na wananchi kupitia upigaji kura. Mangwasha anamweleza Chifu Mshabaha kuwa ukabila hautakuwa na nafasi tena katika jamii yake kwani si chakula ambacho mtu anaweza kupika na kula.

**Mwandishi alivyomsawiri Mwanamke katika Riwaya ya *Nguu za Jadi* (2021) kwa njia hasi.**

**Mwanamke kama ambaye hafai kusikizwa**

Mwandishi amemchora mwanamke kuwa mhusika asiyefaa kusikizwa. Mangwasha alitamanai kufisha uhasama baina ya Wakule na Waketwa lakini nafasi yake katika jamii haingemruhusu.

Mwandishi anatueleza kuwa:

*Mangwasha hakuwa mwanasiasa wala kiongozi wa serikali. Lakini alifahamu mengi kuhusu nchi yake. Alitamani sana kuzungumza na baadhi ya viongozi ili amani idumu nchini Matuo hata kama hakuwa kiongozi serikalini. Alitamani sana kufisha uhasama uliokita mizizi baina ya jamii hizi mbili lakini nafasi yake ya kijamii haikumruhusu. Je, mwanamke angesikizwa katika jamii hii iliyoshiba ubabedume? (uk.7)*

Katika jamii nyingi za Kiafrika, mwanamke huonekana kama mhusika ambaye anafaa kuwepo tu na wala si kusikiliza hata ingawa kile anachokusudia kusema ni muhimu. Mfumo

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

huu wa ubabedume ni dhalilishaji kwa mwanamke. Si kila wakati mwanaume ndiye anayeweza kuwa na mawazo ya kuikomboa jamii yake kutokana na maovu ambayo huenda yakaikabili. Ni vyema basi mwanamke kupewa nafasi ya kuweza kuchangia maendelea ya jamii yake na wala si kuupuzwa kwa misingi ya jinsia yake. Mangwasha anashinda kupewa fursa ya kusikiliza na jamii yake ili kuisadia katika juhudi za kuhakikisha kuna amani baina ya makabila mawili ambayo yalikuwa yakizozania uongozi wan chi ya Matuo.Mtazamo huu ni hasi didhi ya wanajamii wa kike, yaani wananyimwa fursa ya kutoa mchango juu ya suala muhimu la kijamii licha ya suala hilo kuwaathiri wao vilevile.

**Mwanamke kama mpokezi wa athari za tamaduni potovu**

Mwandishi anamchora mwanamke kuwa mara nyingi ndiye hupokeaa athari za tamaduni potovu katika jamii yake. Mwandishi anatueleza kuwa Mangwasha alishindwa kumshauri Lonare kwa sababu ya minyororo ya kitamaduni. Hili linadhihirishwa vizuri na mwandishi namna hii:

*Mangwasha alijua kwamba kupitia kwa Lonare, angekuwa na nafasi ya kuwajulisha Waketwa yale yaliyokuwa yakiendelea afisini mwa chifu. Aidha, alifahamu kwamba daima wanawake walipaswa kusikiliza na kutenda bali si kusikilizwa na kutenda. Lakini lisilo budi hutendwa. Alikataa kabisa kufikiria juu ya hatima yake kwa sasa. Hakujali kujua kule atakakoanzia maisha yake mapya baada ya kutimuliwa Taria.Alielewa Lonare ni kiongozi wao. Hivyo, alipaswa kujulishwa mapema kabla ya maji kuzidi unga. Hapo alisita na kufikiria, "Je, akipuuza nitakalomwambia, hataniona mie ni mwongo tu?" Potelea mbali. Atamwambia, liwalo liwe. (uk.11)*

Katika jamii za Kiafrika mwanamke hana sauti mbele ya mwanamume,mara nyingi mwanamke hulinganishwa kuwa sawa na watoto hivi kwamba hawezi toa kauli mbele ya mwanamume.Mangwasha licha ya kufahamu maovu ambayo yalikuwa yanapangwa dhidi ya Waketwa ofisini mwa Chifu Mshabaha,anashindwa kuenda kumweleza Lonare kwa sababu jamii yake imeweka wazi kuwa wanawake walifaa kusikiliza na kutenda na wala si kusikizwa na kutenda.Mfumo kama huu ni adui mkubwa kwa maendeleo yoyote ya kijamii na kwa hadhi ya mwanamke kama mwanajamii.

**Mwanamke kama muuaji**

Kupitia kwa mhusika Cheiya mwandishi amemchora mwanamke kama mtu anayeweza kutekeleza mauaji. Cheiya anatumiwa na Lesulia ili kumtilia sumu Lonare.Mwandishi analidhihirsha hili hivi:

*Siku ya kuwasilisha vyeti vya uteuzi iliwadia. Lonare akasindikizwa na umati mkubwa wa wafuasi wake. Walipokuwa wakirudi nyumbani, Lonare alitazama nje dirishani akamwona mwanamke aliyekuwa akiongea kwa njia ya simu. Alimtambua.Ndiye aliyetumwa na Lesulia kumwekea sumu katika kinywaji chake. Alimtambua kutokana na alama ya kovu shavuni. Hakuwa amemtajia yeyote habari hizi. Baada ya jaribio hilo, Cheiya alitoweka kama moshi. Hakuonekana hadi wakati huu. (uk 115)*

Maovu mengi katika jamii huwa yanatekelezwa na wanaume kwa kuwatumia wanawake ambao huwa na tamaa kupindukia hasa kuhusu pesa. Cheiya anajipata katika hali hii kwa kukubali kutumiwa na Lesulia ili kumwangamiza Lonare ambaye alikuwa mpinzani wake mkubwa katika uchaguzi wa jimbo lao.

**Mwanamke kama mvunjaji familia**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Familia huwa ndio nguzo kuu ya jamii na kuporomoka kwake mara nyingi hutishia mustakabali wa jamii kwa ujumla. Kupitia kwa mhusika Cheiya mwandishi anamchora mwanamke kuwa ndiye anayechangia kuvunjika kwa asasi hii muhimu katika jamii. Licha ya Cheiya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Mashauri bado anaanzisha uhusiano huu wa kimapenzi na babake Mashauri mzee Sagilu.Jambo hili linatia doa katika uhusiano wa Mashauri na baba yake Sagilu.

Mwandishi analidokeza hili hivi:

*Alimwona babake akishuka kutoka orofa ya juu. Mkononi amemshika Cheiya kama mkoba. Wawili hao walishuka ngazi taratibu. Walikumbatiana na kunong`onezana maneno ambayo ni wao tu waliyafahamu. Mara wasimame kwenye ngazi wacheke. Mara wapigane pambaja. Mashauri alisimama huku akisononeka moyo. Aliwatumbulia macho kama aliyemwona ibilisi na mkewe. Mashauri alitembea taratibu hadi kuwafikia. Aliendelea kuwakodolea macho. Kinywa chake kilikuwa kikavu, kikakosa kutoa neno hata moja. Waliinua vichwa kumtazama. Cheiya alimwachilia mzee huyo, akampita Mashauri mbio na kumpiga kumbo karibu amwangushe. Alimwaga nyayo na kutokomea bila kutamka neno. Alimsikia Mashauri akimuuliza, "Hapa ndio kazini? Nijibu wewe kiokote! Hapa ndio kazini?"*

*Mashauri akamgeukia mzazi wake, "Jinsi nilivyokuheshimu baba leo wanila kivuli? Kazi zote unazonituma kukufanyia, malipo ni haya?" (uk.121)*

Familia kama mojawapo ya asasi muhimu katika jamii inaendelea kukumbwa na changamoto si haba.Changamoto kuu ikiwa ni suala la wenye mahusiano kuwaendea kinyume wapendwao.Licha ya Cheiya kuwa katika mahusiano na Mashauri anakubali kuingia tena katika uhusiano wa kimapenzi na mzee Sagilu baba yake Mashauri.Mashauri anafumania wakitoka mhakawani walikokwenda kufurahia tendo la ndoa.Jambo hili linamuuma sana Mashauri ambaye anafikia uamuzi wa kuvunja uhusiano wa aina yoyote na baba yake hivi kwamba familia hii kusambaratika.

**Mwandishi alivyomsawiri Mwanaume katika Riwaya ya *Nguu za Jadi* (2021) kwa upande hasi.**

**Mwanaume kama katili**

Mwanaume amechorwa na mwandishi kuwa ni mtu katili na asiye na huruma. Tuanalezwa kuwa Sagilu alikuwa katili dhidi ya wale waliokinzana naye kibiashara.

Alijua ukiritimba na hakutaka wengine wampiku kwa lolote. Kwa wale waliomshinda kwa werevu, aliwafanyia hila, mizungu na visanga hata kuwafilisi kabisa kibiashara.

Tunaelezwa hili na mwandishi hivi:

*Sagilu alikuwa na tabia ya kubadilikabadilika kama lumbwi .Wakati mwingine ,alionekana mtanashati na mwingi wa bashasha.Wakati mwingine ,alijaa kiburi na majitapo huku akiwadharau wengine hasa maskini .Alikuwa katili kwa wale waliokinzana naye kibiashara.Alijaa ukiritimba na hakutaka wengine wampiku kwa lolote.Kwa wale waliomshinda kwa werevu,aliwafanyia hila ,kuna wale waliompiku kwa mengine kama vile busara ya maisha.Hawa aliwazuga ,akawatia mfukoni kwa kutumia pesa nyingi alizokuwa akivuna.(uk.16)*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt.Aggrey Wanyama, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Hali ya kutaka kuwa na vitu au sifa zaidi ya vile mtu huhitaji huwafanya wengi wa wanaume kutenda mambo ambayo ni ya kufedhehesha na kukinzana mifumo ya kiutawala iliyopo katika jamii nyingi za Kiafrika.Mhusika Sagilu anadhihirisha hili kwa namna anavyowatenda kinyama wanaoshindana naye katika biashara kwa kuwaua n ahata kuwapokonya mali yao kwa kutumia kifua na nguvu kupita kiasi.

**Mwanaume kama mroho**

Mwandishi amemsawiri mwanaume kuwa mtu mroho na anayejitakia kila kitu. Tunaelezwa kuwa Sagilu anahatarisha maisha ya watoto kwa kuagiza maziwa yaliyotiwa sumu ili yaziweze kuharibika haraka. Mwandishi anadhihirisha hili hivi:

*Raia wa Matuo hawataweza kusahau kisa kimoja ambacho kilitishia maisha ya watoto wachanga kilichosababishwa na Sagilu.Alikuwa ameagiza maziwa ya watoto kutoka nje ya nchi. Maziwa hayo ya unga yalihatarisha maisha ya watoto wote nchini. Hii ni kwa sababu yalitiwa dawa yenye sumu ili yasiharibike haraka. Waliokunywa maziwa hayo walitapika na kuendeshaa kiasi cha kutia nchi nzima taharuki. Hospitali na zahanati zikasheheni watoto wagonjwa hadi wakati ambapo ilibainika kwamba chanzo cha yote hayo ni maziwa. Hakuna alilofanyiwa Sagilu hata baada ya maumbufu hayo. Aidha, alikuwa ameimarisha mtandao wa mafisadi ambao polisi walishindwa kabisa kuuangamiza. (uk.17)*

Wanasiasa wengi katika mataifa yanyoendelea barani Afrika huwa ni wenye kutojali hali za raia wake,wameweka mbele maslahi yao binafsi.Kulingana nao namna ya kujipalia utajiri si tatizo cha muhimu ni kuwa wamepata huo utajiri hali inayopelekea baadhi yao kuweka maisha ya raia wao hatarini.Hulitekeleza hili kwa kuwa na vikundi vya kiuhalifu ambavyo si rahisi kwa polisi wa kawaida kuvitia mbaroni kwa sababu ya vikundi hivi kuwa na uhusiano na maafisa wakuu katika idara ya polisi.Sagilu anadhihirisha hili kwa kuagiza maziwa ambayo anatia kemikali kupita kiasi ili kuyahifadhi,wakati yanapotumiwa na raia wengi wanaendesha hadi kufa.

**Mwanaume kama mkware**

Ukware ni ile hali ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye si mwanadoa mwenzako. Mwanaume amechorwa na mwandishi kama mhusika anayependa anasa kupindukia pasi na kujali athari inayoambatana na tabia hiyo. Tunaelezwa kuwa Sagilu alibadilisha magari sawa na alivyobadilisha wanawake. Alioa mara tatu. Aliwanyang`anya wanaume wengine wake zao. Hakustahimili kumwona mmoja akiwa na mke maridadi.Mwandishi anaeleza hivi:

*Alibadilisha magari sawa na alivyobadilisha wanawake. Alioa mara tatu. Aliwanyang`anya wanaume wengine wake zao. Hakustahimili kumwona mmoja akiwa na mke maridadi. Alimnyemelea na mwishowe kuuvunja unyumba wake. Alijulikana sana Taria kwa sababu hii. Hivyo, hakuna mwanamume aliyeoa aliyempenda Sagilu. (uk.18)*

Wamitila (2002:157) akimnukuu Simone de Beauvoir anaeleza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge.Inamchukulia mwanamke kama kitu hasi naye mwanamume kama binadamu kielelezo.Mwishowe mwanamke anaishia kuwa kama chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni hasi unaomwona mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume.Jamii nyingi zinazoongozwa na mfumo wa kuumeni humpa mwanamke majukumu matatu ambayo ni; kuzaa,kulea na kumstarehesha mwanaume kupitia tendo la ndoa.Hali ni dhalilishaji kwa wanajamii wa jinsia ya kike.Sagilu anathibitisha hili kwa namna anavyowatumia wanawake kuzima kiu chake cha

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt.Aggrey Wanyama, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.

uchu.Kwake yeye,mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanaume.Yuko radhi hata kuwanyang`anya wanaume wenzake wake zao hili tu aweze kulitekeleza hili.

**Mwanaume kama mwenye dharau**

Mwandishi amemchora mwanaume kuwa mtu anayedharau wengine katika jamii anamoishi. Chifu Mshabaha anamdharau Mangwasha na kumwona si lolote. Mwandishi anadokeza hivi:

*Chifu alimtazama kama mzazi aliyekosewa na mwanawe. Kisha alishusha pumzi na kutamka, "Unataka likizo ya nini hasa? Ninaona hukutaja katika barua" Mangwasha alihisi swali hilo halikuwa na maana kwani chifu alijua sababu ya likizo hiyo. "Samahani chifu lakini ni ya matayarisho ya arusi yangu" "Matayarisho…" chifu alitamka huku akigotagota kalamu juu ya meza, "Na baada ya arusi? Hungetaka kwenda kwenye fungate yenu?"*

*Kisha alitoa kicheko cha bezo na kusema, "Naelewa.Hakuna hela za kuwapeleka visiwani au ng`ambo kusheherekea arusi yenu. Zitoke wapi kwa mtu kama yule asiye na satua? Naona mtahitaji wasamaria kama sisi kuja kuwatoa shimoni." (uk.22)*

Utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika zimemkweza mwanaume zaidi huku zikimdidimiza mwanamke.Hili hujitokeza hata kupitia kwa jinsi wahusika wa jinsia ya kike wanavyozungumza na wanawake katika jamii yao.Lugha wanayotumia dhidi yao huwa ni ya kuwakejeli na kuwafanya baadhi kuhoji umuhimu wa wao kuwepo katika jamii hizi.

Chifu Mshabaha anatumia lugha dhalilishaji dhidi yake Mangwasha wakati Mangwasha anaomba ruhusu ya kutohudhuria kazi ili kuweza kujiandaa kwa ajili ya arusi yake na Mrima.Kulingana na Chifu Mshabaha, Mangwasha na mume Mrima hawana uwezo wa kwenda fungate baada ya arusi kwa sababu ni wachochole na hivyo watahitaji msaada wa wasamaria wema ili kutekeleza hilo.

**Mwanaume kama mtu ambaye si mwajibikaji**

Mwandishi vilevile anadhihirisha kuwa mwanaume anayatelekeza majugumu yake katika jamii. Mrima anajitosa katika ulevi na kushindwa kuwajibikia watoto wake.Hili linaelezwa na mwandishi hivi:

*Mrima alianza kushiriki ulevi akawa anakesha katika vilabu vya pombe. Watoto walishinda wakimsumbua mama yao. Walitaka kujua aliko baba yao. Mama hakuwa na jibu ila kuwapumbaza kwa ahadi za uongo. Mwishowe, Mrima alikosa kufika kazini mara kwa mara. Alianza kuheba kazi na kupotelea ulevini. Alipofika nyumbani, alikuwa hatazamiki. Nguo zilikuwa chafu. Zilinuka uvundo wa pombe. Nywele zake zilitimka. Macho yake daima sasa yalikuwa mekundu kama ya mvuta bangi. Haya yalimshangaza Mangwasha sana. Akaanza kuchunguza kilichosababisha mabadiliko hayo ya ghafla ya mumewe. (uk.27)*

Katika jamii nyingi za Kiafrika,baada ya mwanamume kumwoa mwanamke huwa ni kama amepata mfanyakazi wa nyumbani hivyo basi mwanaume huyu hutelekeza wajibu wake.Jambo hili humlazimu mwanamke kuwa mama na baba kwa wakati mmoja jambo ambalo si rahisi.Mrima baada ya kuanza kutumia pombe kwa kupindukia hawajibiki katika kutekeleza wajibu wake pale nyumbani hivi kwamba suala la malezi anamwachia mkewe Mangwasha .Jambo hili si nzuri katika ndoa kwani humfanya mmoja wa wanandoa kuhisi kana kwamba anatumiwa katika mahusiano hayo.

**Mwanaume kama muuaji**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt.Aggrey Wanyama, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.

Chifu Mshabaha anapanga mauaji ya Waketwa. Analitekeleza hili ili kupunguza idadi yao na kuhakikisha kuwa hawangeshinda uchaguzi katika eneo la Ndengoni.Mwandishi anatueleza hivi:

"*Sikiliza Lonare, jana machifu wote wa nchi ya Matuo waliitwa na na Mkuu wa Mji wa Taria kwa kikao cha faragha. Baada ya kikao hicho Chifu Mshabaha aliingia afisini mwake akiwa amebeba majalada kadha. Nyuma yake alifuatiwa na watu watano. Sijawahi kuwaona watu hao. Chifu alifunga mlango wake kwa mazungumzo ya faragha nao," Mangwasha alieleza. "Watu hao walikuwa wamevaa vipi?" "Aah, walivaa shaghalabaghala tu. Yaani bwaga mtwae tu. Hawakuwa nadhifu hata" "Endelea", Lonare aliashiria kwa mkono.*

*"Nilitaka kujua walikuwa wakiongea kuhusu nini. Hivyo nilinyapianyapia nje nikasimama karibu na dirisha lake lililokuwa wazi. Nilimsikia Mshabaha akisema kwa hamaki, "Lazima wahamishwe. La, sivyo, tutakosa mtoto na maji ya moto!"*

*Nilishangaa sana. Kumbe aliyokuwa akizungumzia ni haya unayoniambia!" (uk.55)*

Mwanaume amejidhihirisha katika njia nyingi kuwa anaweza kutumia njia zozote zile kuendeleza utawala wake na kusalia mamlakani. Wengine hufikia hatima ya kuwaua wengine ili kuliafiki hili. Na hivyo kumdhihirisha mwanaume kama mtu muuaji. Chifu Mshabaha anapanga njama ya kuwaua Waketwa ili kupunguza idadi yao na hivyo kumhakikishia Sagilu kushinda uchaguzi. Jambo hili halifai kutukia katika jamii kwani maisha ya mwanadamu ni zaidi ya kuupata uongozi.

**Mwanaume kama msaliti katika ndoa**

Mwandishi anatuonyesha jinsi ambavyo Mrima anaandikiwa barua na wanawake ambao wanamweleza kuwa wanampenda kwa dhati. Jambo hili linatishia kusambaratika kwa ndoa yake na Mshabaha.

Hili linadhihirika hivi:

*Mangwasha alisoma tena na tena. Alijua barua hiyo ilitoka kwa mwanamke. Mwanamke ambaye Kiswahili si lugha yake kutokana na jinsi alivyoandika barua. Mwishowe alishusha pumzi akasem, "Hakika shingo hubeba vyombo, lakini moyo hubeba mambo, tena makubwa. Mrima amekumbatia chui. Hajui chui si rafiki wa kukumbatiwa? Mwishowe atafukarishwa asalie kuguguna vifuu. Hajui dunia ni rangirangile? Acha aendelee kuwabusu nyuki. Siku akiumwa sawasawa, atarejea papa hapa akiramba majeraha", (uk.77)*

Ndoa ni asasi muhimu katika jamii kwani kwa kupitia kwake,familia hupatikana.Licha ya haya,asasi hii imezidi kukumbwa na changamoto kila uchao.Changamoto hii ikiwa suala la wanandoa kuwa na macho ya nje.Jambo hili mara nyingi husababisha kupotea kwa uaminifu baina ya wanandoa na hata wakati mwingine ndoa hizi husambaratika na kumwacha mmoja wa wanandoa ambaye ni mwanaminifu akiwa na machungu ya moyo.Mrima licha ya kuwa ana mke ana uhusiano na wanawake wengine.Wanawake hawa wanamwandikia barua Mrima kwa bahati mbaya ,Mangwasha anaipata barua yenyewe.Tukio hili linamuumiza Mangwasha sana.

**Mwanaume kama msababishaji wa vurugu katika jamii**

Mwanaume amechorwa na mwandishi kuwa ndiye chanzo kikuu cha utokeaji vurugu katika jamii. Sagilu anamtumia Sihaba kusambaza vijikaratasi ambavyo vilieleza Waketwa kuhama sehemu hiyo waliyokuwa wakiishi baada ya kufurushwa makwao.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Hili linabinishwa na mwandishi hivi:

*Alimwona Sihaba akikokotwa ndani ya afisi na polisi wawili. Mkononi ameshikilia vile vijikaratasi vilivyotawanywa pale Matango.Umati mkubwa ulikuwa mahali hapo na ulizidi kutanuka. Watu walikuwa wamepandwa na mori. Walipaaza sauti wakisema aachiliwe ili wao wenyewe wamwadhibu. "Itakuwaje mwanamke huyu atumwe na mtu kusambaza vijikaratasi? Huyu ni kibaraka wa mtu fulani wala si serikali!" alisema mtu mmoja aliyepandwa mori.*

*"Leo tunataka kujua mbivu na mbichi. Atuambie ardhi ni ya nani hasa", mwingine alidakia. Kila mtu alikuwa na lake la kusema. Maswali yakazidi na hakuna aliyekuwa na jibu. Sihaba alifumba kinywa. Hakutaka lolote hata baada ya kushambuliwa na wenyeji wa Matango.Alifungiwa ndani. Watu wakalazimishwa na askari polisi waende zao hadi uchunguzi ufanywe. Miongoni mwao, alikuwa Mangwasha na rafikize.*

*Mangwasha alipomwona Sagili mahali hapo, moyo ulimwenda mbio. Alimfuata pamoja na kundi la watu. Sagilu alipowaona wakimjia. aliingia ndani ya gari lake akatoka mbio. (uk.79)*

**Mwanaume kama msaliti wa mabadiliko katika jamii**

Mwandishi anamchora mwanaume kuwa ndiye asiyetaka kuwepo na mageuzi katika jamii. Hususan katika utawala. Mrima anasaliti jitihada za wananchi wenzake za kutaka kujinasua kutoka katika uongozi dhalimu kwa kumuunga na kuendesha kampeni za Sagilu.Hili linadhihirishwa hivi:

*Alimshukuru pia kwa kukubali kuharibu na kufunga njia zote za Mwamba ili Sagilu apate ushindi katika uchaguzi ujao. Hapo ndipo alipomtaka Mrima kupokea pesa zile shilingi elfu mia nane taslimu kutoka kwa mtemi.*

*Aliahidiwa zingine kiasi kama hicho mtemi atakapoona dalili ya bidi yake. Alishauriwa kuwa makini ili mkewe au hata rafikize wasijue mipango hii. (uk.110)*

Mabadiliko katika jamii nyingi za Kiafrika mara nyingi hukosa kuafikiwa kwa sababu ya ubinafsi wa viongozi wachache ambao wangependa mfumo dhalimu uliopo kuendelea kwa manufaa yao wenyewe.Ili kuhakikisha hili halitimii wengi wao hutumia mbinu nyingi zikiwemo kuwahonga raia ili kuwachagua na hivyo basi kudumisha mfumo wa kiutawala uliopo.Mrima anatumiwa kutekeleza hili na Chifu Mshabaha kwa kulipwa hela nyingi na kuhadiwa nyingine endapo juhudi zake zingefua dafu.Si vizuri kwa baadhi ya raia kuwa mstari wa mbele kupinga mabadiliko ambayo labda yangeleta afueni wa raia wake ambao wanazidi kuumia kutokana na utawala gandamizaji.

**Mwanaume kama mvunja mila**

Mwanaume amesawiriwa kuwa ndiye anayevunja mila katika jamii. Mwandishi anatueleza kuwa Sagilu alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Cheiya anayedhaniwa kuwa mkaza mwana wake. Cheiya alikuwa akichumbiana na Mshauri mwanawe Sagilu. Hili tunaelezwa hivi:

*Aghalabu, Cheiya alikuwa akimfahamisha Mashauri kila alipoandamana na babake kwenda kuzuru mji. Mashauri hakujali sana. Alielewa kwamba babake aliinukia kumpenda Cheiya kama mwanawe. Alimpenda kama binti ambaye hakujaaliwa kupata. (uk.118)*

Jamii nyingi za Kiafrika huthamini sana utamaduni kwa kiasi kwamba wale wanaoenda kinyume na utamaduni huu uonekana kama waasi japo kuna baadhi ya wanajamii ambao

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

hutokea kuvunja tamaduni hizi kwa sababu za kibinafsi.Sagilu baba yake Mashauri ni mmoja wao wa wanajamii ambao wanaenda kinyume na tamaduni za jamii yake.Sigula licha ya kufahamu kuwa Cheiya alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanawe Mashauri bado anamshawishi kushiriki mapenzi.Jambo hili linapelekea uhusiano baina ya Cheiya na Mashauri kuvunjika,pia Mashauri anakataa kumwita Sagilu baba tena.Kulingana na mwandishi,ni wazi kuwa mwanaume ndiye huwa mvunjaji wa mila katika jamii yake kwa kutenda vitendo ambavyo anafahamu wazi kuwa ni mwiko katika jamii yake.

**Mwanaume kama kiongozi mbaya**

Mwandishi amemchora mwanaume kama kiongozi mbaya. Uongozi mbaya serikalini unaonekana kupitia kwa Mtemi Lesulia ambaye alitawala kwa mkono wa chuma. Hili linaonyeshwa hivi:

*Mtemi Lesulia alitawla kwa mkono wa chuma. Aghalabu, kauli alizotoa zilichukuliwa kama sheria za nchi. Wengi walimwogopa. (uk.7)*

Katika jamii nyingi ambazo huongozwa na mfumo wa kuumeni,mwanaume huchukuliwa ndiye kiongozi wa jamii yake na hivyo kupewa heshima stahiki nafasi hii.Wakati mwingine viongozi hawa huruhusu nguvu za utawala kuwaingia katika vichwa vyao na hivyo basi kutawala wanajamii kwa kutumia mguu wa kausha,wakati mwingine viongozi hawa uwaua wapinzani wao ili kusalia uongozini.Mtemi Lesulia anadhihirisha hili kwa namna anavyotawala raia kwa kutumia mkono wa chuma.Utawala wake unamfanya yeye kuogopewa na raia wake.Mwandishi vilevile anashadidia hili namna hii:

*Wakati mmoja, Mangwasha alitaka kukutana na Mtemi Lesulia.Alipomtajia hili, huyu alidhani mkewe karukwa na akili. Alishangaa ujasiri huo aliutoa wapi. Akamkanywa asiruhusu wazo kama hilo akilini mwake. Mangwasha alielewa, akaliondoa wazo kama hilo akilini mwake. Mangwasha alielewa akaliondoa wazo hilo katika fikra zake.*

*Yeye alikuwa mhazili tu aliyeajiriwa katika afisi ya Chifu Mshabaha.Si lolote si chochote mbele ya chifu huyo aliyetoka katika jamii ya Wakule. (uk.8)*

Kuna wakati Mangwasha alitaka kukutana na Mtemi Lesulia, Lonare anaondokea kumwonya Mangwasha kutokeleza jambo kama hilo, kwa upande wake Lonare, Mtemi Lesulia alikuwa kiongozi dhalimu ambaye alikuwa ameyatekeleza maovu mengi dhidi ya raia wake ambao alifaa kuwaongoza.

**Mwandishi alivyomsawiri Mwanamume katika Riwaya ya *Nguu za Jadi* (2021) kwa upande chanya.**

**Mwnanaume kama mtetezi**

Mwanaume amesawiriwa pia kuwa mtetezi. Lonare anawaeleza akina Mangwasha kuwa inafaa taarifa za kushambuliwa kwa Waketwa kusambazwa haraka ili kuweza kutibua njama ya Wakule ya kuitekeleza.Mwandishi anadhihirisha hivi:

*"Yale anayonuia kuwafanyia watu wangu yatamtumbukia nyongo", Lonare alitamka na kucheka. (uk.56)*

**Mwandishi alivyomsawiri mwanamke katika Riwaya ya Nyuso za Mwanamke kwa upande hasi.**

**Mwanamke kama asiye na uwezo wa kujifanyia maamuzi.**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama, **
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


Jamii nyingi duniani,hasa zinzofuata mfumo dume,mwanamke amekuwa akitazamwa kama kiumbe duni asiyekuwa na uwezo wa kufanya uamuzi.Nafasi yake imekuwa ikiwekwa katika ufinyu wa kimawanda tofauti na anavyotazamwa mwanaume (Mbughuni,1982).Kwa Waafrika,ambako jamii nyingi zinatawaliwa na mfumo dume,uwezo wa kufanya uamuzi kwa jinsia ya kike umekuwa ukiminywa katika maeneo mbalimbali.Miongoni mwayo ni masuala ya ndoa ambazo kwa kiasi kikubwa zinafungamanishwa na matakwa ya mila,desturi,itikadi pamoja na falsafa inayotawala maisha yao.Waafrika wanaamini kuwa mwanamke au binti aliyefikia umri wa kuolewa hana uwezo mzuri wa kiutambuzi kati ya jema na baya.Maisha yake yamekitwa katika misingi ya kuongozwa na kuchaguliwa lililo zuri na kuepushwa na baya.Katika muktadha unaofumbatwa na itikadi pamoja na mila na desturi za Mwafrika, hiyari ya mtoto wa kike ni kukubaliana na uamuzi unaofanywa na wazazi wake au unaotokana na jamii na si vinginevyo. Hapa ndipo huvikwa uso kama kiumbe dhaifu asiyeweza kufanya uamuzi sahihi kwani hana hiyari ya kufanya uamuzi kulingana na utashi wake. Wanaufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa ndoa kama asasi mojawapo ya utamaduni ina mchango mkubwa katika kumdhalilisha mwanamke, hasa kutokana na pingu inazomtia utumwani; hivyo, kumnyima uhuru wa kufanya uamuzi binafsi.Hapa mwanamke anatakiwa awe mtii na kukubaliana na kila linaloamuliwa na wazazi au jamii yake.Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*,mwandishi amemsawiri mwanamke kama kiumbe asiyeweza kufanya uamuzi binafsi.Hili linadhihirika kupitia madhila mbalimbali wanayokumbana nayo wanawake kwa kuchaguliwa wenza na wazazi ili kukidhi matakwa ya jamii na hulazimika kutii, kwani hana uwezo wa kufanya uamuzi kulingana na misingi ya jamii.Mfano mzuri ni mhusika *Bi.Mkubwa* (mama yake Nana), anayechaguliwa mume wa kuishi naye.Kwa kuhofia kukiuka matakwa ya wazazi wake,anaamua kuolewa bila kuwa na mapenzi na yule aliyemuoa.Haya yanabainishwa na Nana pale anaposema kuwa:

*“Mimi sitataka kuchaguliwa kama alivyochaguliwa mama`angu”.Uk.42*

Mhusika mwingine anayeangaliwa kama kiumbe asiyeweza kufanya uamuzi binafsi ni Shemsa. Anatii kila jambo analoambiwa na kuamuliwa na wazazi wake. Hii inatokana na mifumo ya jamii aliyomo ambayo imemlea na kumkuza. Ingawa hakutaka kuolewa na Sadiki mchumba aliyechaguliwa na wazazi wake, minyororo ya desturi inamfunga na kumlazimisha kutii sheria na mamlaka kama anavyotueleza Bi. Kivumbasi:

*…hapa petu mwanamke haposi, huposwa; na anapoposwa akikataa huwa jambo kubwa ikiwa familia yake wanataka binti yao aolewe na huyo mwanaume aliyekuja kuposa. Basi kinyume cha mambo,huwa mwanaume wanayemtaka wao siye anayemtaka binti yao.Ikiwa binti yao atamkataa mwanaume wanayemtaka wao,basi wazee watatumia kila hila ,na hila zikishindwa nguvu hazikufanya kazi,hutumia msusio…hapa petu mwanamke hawezi kumkataa mwanamume anayemposa hata kama hamtaki.Uk.208*

Mwandishi pia anatuonyesha kuwa uamuzi wowote katika jamii zinazotawaliwa na mfumo dume uko chini ya mamlaka ya mwanaume.Katika muktadha huu,mwanamke hubaki kuitikia hewala kwa kila analoamuliwa.Hana nafasi ya kutoa ushauri wowote katika jamii hata ikiwa anahusika moja kwa moja na suala linalohitaji ufumbuzi.Siku zote amekuwa mnyenyekevu kwa kutaka suluhu na salama yake anayoipata ndani ya utii uliojengwa na wigo wa jamii.Jambo hili linajibainisha katika kisa cha Bi.Mau anaposimulia namna mke alivyompa ushauri mumewe wa kutomwozesha binti yake kwa mumw asiyemtaka.Matokeo yake, mume alimuona mkewe kuwa mpumbavu kwa ushauri wake.

**Mwanamke kama asiyefaa kuwa kiongozi.**

Kama zilivyo jamii nyingine duniani, jamii ya Kiafrika pia huzingatia mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia jinsia baina ya wanawake na wanaume. Suala la uongozi huzingatia mfumo huo, ambapo mwanamke hutazamwa kama kiumbe asiyeweza kuiongoza jamii (Haji,2014). Nafasi yake huwekwa katika kiwango cha familia ambapo hupewa jukumu

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

la uzazi na ulezi wa familia.Haji (khj) anaeleza kuwa katika jamii zenye mfumo dume,hususani jamii nyingi za Kiafrika,mtoto wa kiume huandaliwa kuwa shujaa na kushika nafasi za uongozi huku mtoto wa kike akiandaliwa kuwa mama na mlezi wa familia.Katika mtazamo huu,waandishi wa kazi za fasihi wamekuwa wakimsawiri mwanamke kama kiumbe duni kwa kumuweka katika daraja la chini.Hii ni pamoja na kumpa majukumu ambayo yanaonekana kuwa mepesi na ya mawanda ya familia. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanmke*, Nana anabainisha hili kwa kusema:

*…maisha yetu wanawake hapa petu yamefinyangwa ndani ya tamaduni zilizoasisiwa na mwanamme ambazo bado zina nguvu kubwa kupita kiasi. Zinafanana na tamaduni za the untouchable ambamo waliozaliwa vinyozi wanabaki kuwa vinyozi mpaka wajikekete nyembe na kujimaliza wao wenyewe; wanaokuja duniani wapishi, wapike bondo maisha yao yote, mpaka moshi uwasonge kooni kuwaziba pumzi wao wenyewe; wanaotokana na koo za wakulima wainue na kushusha majembe siku zote…(uk.107)*

Ni wazi kuwa mwanamume hujificha chini ya tamaduni gandamizaji ili kuendeleza hujuma dhidi ya mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika.Mwanamke kwa sababu ya kutokwa na uwezo wa kukabiliana na tamaduni hizi,husalia kuwa mwombezi wa mwanaume ili asionekana kama ayekwenda kinyume na itikadi hizi.Maoni haya yanaunga mkono maoni yake Wamitila(2002:157) akimnukuu Simone de Beauvoir ambaye anasema kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge.Inamchukulia mwanamke kama kitu hasi naye mwanaume kama binadamu kielelezo. Hivi kwamba mwanaume hutumia fursa hii kuendeleza unyanyapa dhidi yake.Jinsi Nana anavyodokeza kuwa mwanamke anayejipata katika tamaduni hizi hana lake,kwake yeye ni sawa na vinyozi waliozaliwa katika utamaduni wa vinyozi na hivi kwamba watasalia katika hali hiyo hadi wajikekete kwa nyembe na kujimaliza wao wenyewe.Licha ya haya,mwanamke ana uwezo wa kujiondoa katika hali pindi atakapofahamu madhila anayoyapitia na kuwa tayari kupambana nayo ili kujinyakulia uhuru wake kutoka kwa mwanaume anayetumia kisingizio cha tamaduni kuendelea kumdhulumu.

**Mwanamke kama asiye na uwezo wa kiuchumi**

Katika jamii, mwanamke amekuwa akitazamwa kama kiumbe tegemezi anayetakiwa kuhudumiwa na si kuchangia katika huduma wala yeye kuhudumia.Kwa mujibu wa Wana ufeministi wa Kiafrika, mtazamo huu umekuwa ukirudisha nyuma maendeleo ya jamii, kwani kutokana na mfumo unaowekwa, mwanamke amekuwa akipewa nafasi finyu katika kuchangia maendeleo hayo (Kitundu,2012)Mwandishi anaonesha hili pale Nana anapomwelezea mama yake wa kambo kama mwanamke tegemezi anayetegemea kufanyiwa kila kitu na mumewe pasipo yeye kujishughulisha. Anasema:

*Mimi (nisikilize vizuri), licha ya kutotaka kubaki jikoni kupika na kupakua, kuosha vyombo na kufagia na kutunza watoto, sitaki mimi kamwe hata kuwa mwanamke kwa maana ya mwanamke anayetunzwa na kulindwa na mwanamume kama mamangu wa kambo au mwanamke hohehahe anayefonzwa damu taratibu, huku akimaliza kama alivyomalizika mamangu mzazi. (uk.109)*

Kulingana na Engels (1975),chanzo cha historia ya kunyonywa na kukandamizwa kwa wanawake ilianza wakati jamii ya binadamu ilipogawanyika katika matabaka mbalimbali.Jamii asilia ilikuwa na uthamini sawa wa kazi za wanaume na wanawake.Jamii

ilipobadilika na kuwa ya kitabaka,ilianzisha urithi upande wa baba.Kutokana na ugawaji wa majukumu kazi za upande wa wanaume zilileta faida zaidi kushinda zile za wanawake.Kutokana na haya,umilikaji wa mali ulimwendea mwanamume ukiwemo pia uzalishaji mali.Naye mwanamke alijitambulisha na majukumu ya uzazi na malezi.Hapa mwanamke alifaidika ingawa hangeweza kutoa uamuzi wowote kuhusu mali isiyo yake.Nafasi ya mwanamke iliendelea kuwa nyuma kutokana na tofauti za kikazi.Tangu jadi jamii ikafunzwa kuamini kuwa mahali panapofaa mwanamke ni nyumbani na ulezi wa watoto(Figes 1978).Mawazo haya yanatiliwa nguuv na Adrienne Rich akinukuliwa na Tong (1989:87) anapoeleza;

*Hadi hivi majuzi mfumo wa kuumeni umefanya mwanamke kuamini kuwa kuzaa ndio kazi yake ya pekee. (Tafsiri ya mtafiti)*

Itikadi hii ingali imeshika mzizi katika jamii nyingi za Kiafrika.Huku kuongezeka kwa mali upande wa baba kulizusha dhana ya kuwepo mali ya kibinafsi. Mwanamume akizidishwa umuhimu kuliko mwanamke. Kiuchumi mwanamume akategemewa na mwanamke. Huu ukawa ndio mwanzo wa mwanamume kutenda lolote juu ya mwanamke anayemtegemea.

**Mwanamke kama mpogezi wa kichapo kwa kuenda kinyume na matakwa ya mwanaume**

Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa ndiye anayepokea kichapo kwa sababu ya jinsia yake kutoka kwa mwanaume pindi anapojaribu kuenda kinyume na kile anachokitaka mwanaume katika jamii nyngi za Kiafrika.Nana anachapwa kofi shavuni na babake kwa kukataa kuolewa na Dusa. Licha ya Dusa kumletea zawadi ya gari aina ya *Volvo*katika sherehe za ukumbusho wa kuzaliwa kwake. Mwandishi anasema hivi:

*Amenizaba kibao baba! Amenizaba.Kibao amenizaba. Kinauma.Maumivu yake ya milele. Kimeniota shavuni. Alama yake haifutiki. Haifutiki kabisa. "Kwa nini? Kwa nini umenipiga baba?""Wewe sawasawa na mama`ako" Aliniambia.Mimi sawasawa na mamangu? Ilinishitusha sana kauli hiyo. Mimi sawasawa na mamangu kwa vipi? Kwa utukutu wangu labda? Kwa kukataa na kususia kwangu? Kwa kutetea haki yangu? Kwa kuhalifu amri? Nilijiuliza hivyo kwa sababu mimi simjui mamangu. Sikumwaona kwa ukinaifu. Sikukutana naye kwe-nye smaku ya miili yetu, sikwambii smaku za roho zetu. Sikuwahi kumjua kusema kweli. Hajawahi kunijua pia. Wala sijui alihitalifiana na babangu vipi. Sitambui kwa namna gani hakufuata amri zake. Inakuaje basi mimi kufanana na mamangu?*

*Kwa huku kukataa kwangu baba kunichagulia njia ya kupita au rafiki wa kufwatana naye kwenye njia hiyo? Mimi ninayemkataa katakata Dusa awe mwenzi wa kuishi name milele. Wa kulala naye kitanda kimoja. Dusa ni kijana mwenzangu ndiyo, lakini sikumchagua. Nimechaguliwa na babangu awe mchumba wangu na hatimaye mume wangu. Dusa kijana mtukutu. Babake ni kizito mwenzetu ndiyo lakini…(uk.44)*

Kwa mujibu wa itikadi za Kiafrika, nafasi ya mwanamke katika jamii ni kuolewa. Katika kulitekeleza hili,mapenzi hayathaminiwa katika uchaguzi wa wachumba.Wasichana hupozwa na hata kuozwa kwa mume aliyechaguliwa na wazazi wake.Tunaona namna Nana anavyolazimishwa kuolewa na Dusa,wakati Nana anapokataa anachapwa kofi na babake.Dusa alikuwa amemletea zawadi Nana gari aina ya Volvo.Kulingana na Nana hakuwa na ufahamu kumhusu Dusa,japo alimletea gari.Nana anakataa kuolewa naye kwa kusema kuwa hakumchagua yeye licha ya kuwa ni kijana mwenzake.Ufeministi wa Kiafrika unapinga suala la mwanamke kutokuwa na uwezo wa kuchagua mume atakayeishi naye.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

**Mwanamke kama mhusika aliyedharauliwa**

Dharau ni tabia ya kupuuza na kutoheshimu watu. Dhana hii ya dharau imetumiwa ili kumtweza mwanamke. Kwa jumla kudharauliwa kunajumlisha kutothaminiwa, kuvunjiwa heshima na kuaibishwa kupitia vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake. Mwandishi anatueleza kuwa Fatuma alinajisiwa na mjomba wake akiwa mtoto mdogo na hata alipokuwa mkubwa. Hata hivyo mjomba mwenyewe alimtishia asiseme. Fatuma alipopata mimba, wazee wa ukoo huo walimsingizia kuwa aliipata mimba hiyo mahali pengine. Tunaelezwa kuwa yeye aliwatoa watu machozi pale alipohadithia jinsi alivyonajisiwa na mjomba wake na kuendelea. Hili linadhihirika hivi.

*"…Hakuna hata mmoja aliyethubutu kumkabili huyo mjomba." (uk.211)*

Hii ina maana kuwa wanaume wanajiona bora zaidi kuliko wanawake. Hii ni kwa sababu ya mfumo wa ubabe dume. Hili huwafanya wanaume kuwadhulumu wanawake ambao kulingana na mtazamo wao wa kuwaona wanawake ni viumbe dhaifu. Kwa kipindi kirefu, mwanamke amenyanyasua kwa sababu ya jinsia yake ambayo imekuwa kigezo cha kutumiwa na chombo cha kumstarehesha mwanamume kwa hiari au kulazimishwa. Mwandishi anatuonyesha namna Fatuma anvyonajisiwa na mjomba wake ambaye anamshurutisha kunyamaza licha ya uovu aliomtendea. Mwanamke ana haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa kwani anachangia pakubwa katika maendeleo ya jamii kwa kutoa maoni na kuchuma mali katika jamii. Dharau inajitokeza pale ambapo mwanamke anakosa kudhaminiwa, kuvunjiwa heshima na kuaibishwa kupitia vitendo anavyotendewa au lugha anaoelekezewa.

**Mwanamke kama asiyefaa kurithi mali ya wazazi.**

Msimulizi anatueleza kuwa anachukia tabia iliyo katika jamii yake ya mwanamke kuwa mwanamke kwa namna mbalimbali zinazopangwa na mwanaume. Mwandishi anaeleza hivi:

*Nikifumbua macho kutazama kila upande ndani ya jamii yangu,huchukia mno tabia hii ya mwanamke kuwa mwanamke kwa namna mbalimbali zinazopangwa na mwanamme.Huichukia mno tabia hii mpaka baadhi ya siku hunitunga hamu ya kutaka niwe Mohammed Ahmed,mhusika wa Mtoto wa Mchanga,yaani The Sand Child na Usiku Mtakatif,The SacredNight,riwaya za Tahar Ben Jellon.Mhusika mkuu mwanamke aliyebatizwa uume na kukuzwa kibarubaru na babake.Kukuzwa kwa hila hii na ile kabla hata tete ya mimba haikudungwa kwenye fuko la uzazi la mamake.Kabla hata mimba yake kufikiriwa ,kwa sababu babake amechoka kuzilea mimba za mabinti saba waliozaliwa kwa uchungu wa kuwa wanawake na kwa hivyo kukatisha tamaa yake.*

*Kwa sababu wanawake saba hao waliozaliwa wasingerithi mali nyingi ya baba yao iliyokuwa haina mipaka. Badala yake mali ingekwenda kwa mtoto au watoto wa kiume wa ndugu wa kiume wa baba mtu. (uk.106)*

Katika jamii nyingi za Kiafrika mwanamke huonwa duni kiasi cha kwamba hawezi kupewa fursa ya kurithi mali ya wazazi wake. Suala la mwanamke kuzaa mtoto wa kiume katika ndoa huwa limetiliwa maanani sana hivi kwamba mwanaume katika ndoa hii huona fahari pindi anapopata mtoto wa kiume kutoka kwa mke wake. Jambo hili linamsababishia msimulizi kutamani kuwa angezaliwa mwanamume ili kuepuka ukandamizaji ambao watoto wa jinsia ya kike wanapitia katika jamii.

**Mwanamke kama mkata tamaa.**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Mwanamke amesawiriwa na mwandishi kuwa mhusika anayekataa tamaa pindi anapokumbana na changamoto katika maisha yake ya kila siku. Tunaelezwa kuwa katika juhudi za kupata uhuru wa kibinafsi, Nana anakata tamaa. Nana hapo awali alikuwa amekoseshwa uhuru na babake Bw. Hila.Jambo hili linamsababishia mateso hususan ya kisaikolojia. Kwake yeye dunia imefika hatima yake. Anaeleza katika Uk.62 kuwa:

*"(De)pression!" Nilimsikia bwana-mpiga-gita akiwaambia wanawake walionizunguka wakiashiria kujipa tamaa pasi na tamaa ya kuibuka kwangu tena…"*

**Mwanamke kama chombo starehe kwa mwanaume**

Bw. Hila anaamini kuwa maisha ya mwanamke ni kustareheshwa, kupewa kila kitu anachokitaka apewe mawazo ya kifahari nay eye kama mwanamke abaki kungoja kumstarehesha bwana na kubaki ndani ya nyumba. Mwandishi analidhihirisha hivi:

*Na hapo Bi.Mkubwa akaanza kuhadithia maisha yake na mwanaume na masiha yake ya ndoa.Alimwambia Nana kwamba licha ya kwamba yeye kaozwa Bwnana Hila kwa nguvu za utajiri na mali yake (kwa sababu yeye hakumtaka), bwana huyo alidhani tu maisha ya mwanamke ni kustareheshwa.Mwanamke ni pampo tu la nyumba kwa hivyo anachostahiki ni kupewa kila kitu alichokitaka ispokuwa kutoka nje ya nyumba.Apewe mavazi ya fahari,manukato ghali,chakula cha rutuba,watumishi wa kila kitu mpaka wa kumfulia chupi zake.Gari la kusafiria na bwana,pesa za masurufu au kununulia anachopenda…(uk.287)*

Jamii nyingi za Kiafrika humpa mwanamke wa Kiafrika majukumu matatu kama vile kuzaa, kulea na kumstarehesha mwanaume. Majukumu haya huwa sawa na kumdunimsha mwanamke. Kulingana na Bi, Mkubwa baada ya kuozwa kwa Bwana Hila, bwana huyu aliona maisha ya mwanamke ni kustareheshwa kwa kupewa kila kitu anachostahiki. Kwa upande wake mwanamke jukumu lake likiwa ni kumpa starehe mwanamume kupindia tendo la ndoa wakati wowote ambapo mwanamume angetaka.

**Mwanamke kama mhusika ambaye ana upweke**

Nana aliishia kuumia katika lindi la upweke aliponyimwa kutoka nje pekee na kutangamana na watoto wa rika lake na pia kujifunza mengi kutokana na mwingiliano wa watu wa pale janibuni pao. Aliishia kuwa pweke kama mfungwa. Jambo hili lilimuudhi mno na ndipo akaamua kujinasua. Anasema hivi:

*"Fikra hii ya kuishi pekee yangu ilinitisha ingawaje kabla ya chagizo za ndani kwa ndani hazikunijia kunishawishi kwa mara ya kwanza kutoroka kwetu. Haikupata kunipitikia akilini mwangu kama ingekuja siku mimi intake kuwa mbali na watu wa jumba hili, ili niishi huru pekee yangu." (uk.32)*

Suala la kuwatawisha wanawake lipo katika jamii nyingi za Kiafrika, hili mara nyingi hutokea wakati msichana amebaleghe hivi kwa familia yake huona itakuwa ni hatari endapo ataruhusiwa kwenda nje na kutagusana na watu wa rika lake. Kwani kulingana nao huenda akaanza kujifunza tabia mbaya kama vile kushiriki ngono na kuuvunja ubikra ambao jamii huenzi na hivyo kuiletea familia yake aibu wakati anapoozwa.

**Mwandishi alivyomsawiri mwanamke katika Riwaya ya Nyuso za Mwanamke kwa upande chanya.**

**Mwanamke kama jasiri.**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt.Aggrey Wanyama, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.

Mwandishi amemchora mhusika mwanamke kama jasiri asiyeogopa, pindi kunapotokea tatizo anaamua kuchukua hatua ili kutafuta uhuru wake.Bi. Mkubwa anatengana na mume wa kwanza ambaye ni Bw. Hila. Bi. Mkubwa anamwona kama mtu dhulumati. Kwa hivyo anaolewa mara ya pili na mume ambaye kiboko kilikuwa kiamsha kinywa chake. Tunaelezwa hivi:

*...Bi.Mkubwa akaanza kuhadthia maisha yake na waume na maisha yake ya ndoa. Mwanamke ni pambo tu la nyumba kwa hivyo anachostahiki ni kupewa kila kitu alichokitaka isipokuwa kutoka nje ya nyumba. Apewe mavazi ya kifahari, manukato ghali, chakula cha rutuba, watumishi, gari la kusafiri na bwana…" (uk.287)*

Bi. Mkubwa anafikia uamuzi wa kukimbia ndoa yake kwa sababu dhuluma aliyokuwa akiipokea humo. Japo halikuwa jambo rahisi kufikia uamuzi huo, ila Bi. Mkubwa aliona ni afadhali kuondoka katika ndoa hii licha kuwa alikuwa akipokea kila kitu kutoka kwa Bw. Hila. **Mwanamke kama mwenye kujitegemea**

Katika jamii ,mwanamke amekuwa akitazamwa kama kiumbe tegemezi anayetakiwa kuhudumiwa na si kuchangia katika huduma wala yeye kuhudumia.Kwa mujibu wa Wana ufeministi wa Kiafrika,mtazamo huu umekuwa ukirudisha nyuma maendeleo ya jamii,kwani kutokana na mfumo unaowekwa ,mwanamke amekuwa akipewa nafasi finyu katika kuchangia maendeleo yao (Kitundu,2012).Hata hivyo,kumekuwepo na jitihada za mwanamke kujitegema katika jamii.Jambo hili linamfanya akwepe hata misaada mbalimbali ambayo ingemfanya kuwa mtegemezi kwa namna moja au nyingine.Nana anakata msaada wowote kutoka kwa Faisal ili kuweza kusimamisha muziki wake wa taarabu.Kama mwanamke,anatumia uwezo wake wa akili na kusimama .Hata pale muziki wa taarabu unapopigwa vita na kuonekana ni haramu kuimbwa na mwanamke,anasimama imara kupigana vita vya kiuchumi vinavyoweka mipaka baina ya mwanamke na mwanaume.

**Mwanamke kama kiongozi**

Licha ya mifumo ya kijamii kumweka mwanamke katika daraja la chini,tunaona namna mwandishi anavyomchora mwanamke kama kiongozi mwenye uwezo mkubwa wa kuongoza.Kama ambavyo Wanaufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa ukombozi wa mwanamke uko mikononi mwa mwanamke mwenyewe.Tunaonyeshwa namna Bi.Chuma anavyoamua kutupilia mbali mtazamo wa ubabedume kuwa kiongozi wa familia ni mwanamume.Mhusika huyu anaamua kutekeleza majukumu mbalimbali ya familia pasipo kutetereka,tofauti na mipaka aliyowekewa na jamii.Mwandishi anatueleza ujasiri na ushupavu wake katika kuiongoza familia yake kwa kusema kuwa:

*…Na yeye, kusema kweli, amechoka kukaa katika nyumba hii ya pamoja inayoongozwa na Bi. Chuma, yule mwanamke shupavu, shujaa na mwerevu. Na kwa upande wake yeye alichoka kuona dunia yake inaongozwa na Faisal. (158)*

**Mwanamke kama mdadisi na mpekuzi wa mambo**

Nana anajitokeza kuwa na udadisi mwingi wa mambo kwa sababu ya mambo aliyokumabana nayo. Kufanya huku ni kujihakikisha ukweli juu ya kile alikuwa anataka kutekeleza. Kwa mara nyingi mwanadamu amejipata katika njia panda kwa sababu ya kutohoji masuala mengi ambayo ana nia ya kushiriki. Suala la kudadisi huku masuala huwa ni njia mojawapo ya

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

kupata uhakika wa jambo na kuondoa dukuduku ya aina yoyote ile. Hili linabainshwa na mwandsihi wakati Nana anamuuliza Amour hivi:

*"Nini msimamo wako kuhusu kuwa na mwenako?" Mwanamke nakusudia…Kuwa na mwenzi maana yake ni nini kwako? (uk.264)*

Kutokana na swali hili Nana aliweza kupata majibu aliyotarajia kupata kutoka kwa Amour maana hakutaka kung`ang`ania mpenzi ambayo hakuyaelewa aidha udadisi wake ulikuwa mizani ya kujua kama Amour alimpenda kwa dhati.

**Mwanamke kama mwenyehurumanaasiyenaubinafsi**

Katikauk wa198Nanaamekirikuwahamu yake ni kuitumikia jamiiyaketutofautinawafanyavyowatuwenginealiokuwaakuwaonanakuwalaumukwa roho.Katikakufanyahivyoanatakakuithibitishiadunia kwambamwanamkeanawezakufanyamambomakubwa.Aidhakwakuisaidiajamiini njiayakujitoleakwaajiliyafahariya mamakealiyekufakifochaaibualichotwikwana dunia.Aliaminikuwainawezakana kujengautajiribilakuwekamaslahiyakembele. Niani kuendeshambelehajazawatuwengiwanchiyakewenyedhikinyingikama mchanga. Nanahanahajayakujengamabaaauvilabuvyapombeaumadanguro,hoteli zawatalii,kumbizamuzikiunaotiachachawizovijanaaumadukayavipodozinanguo zakuwafanyawatuvikaragosinawendatupu. Kwake hatakikufanyahivyokwauhuruwakuuzana kuuziwa balihajayakenikutafutamwenendo wabusarakatikanchiiliwatuwapatekazinawachumepesaza halalizitakazowaendesha waowenyewepamojanafamiliazao."Hivyomambohaya yakifaulunchiitakuwanaamaninakilamtuatamheshimumwenzakenamwanyabaina yawakwasina mahawindeutafinyika."VilevileNanakatikauk.212anasisitizakuwa, tokeaahamekwaojamiiimemfunza kwambamtuhawezikuendambelekwakujali nafsi yaketuhataakijaribukuipajamii mgongo hatapatautulivumaadamhatiaitambezaauitamdharau.

**Mwanamke kama mwenye moyo wa kujirudia na mnyenyekevu**

KwasikukadhaaNanana Faisal walikuwahawasemezani kiinichahasirayaNananikulekuambiwaukwelikwamba hakunasikuBimkubwayani mamakealikujakamamzukanakuhudhuriamjadalawa dukuduku balialiyekuwa akiongeaalikuwaNanamwenyewe nakamaNana alionahivyoilikuwanindototubaadayeNanaalikubalimaelezoya Faisalnahapoakataka waurejesheuhusianowaokamahapomwanzo. Nana anasema hivi:

*"ka kukutolea maneno makali kuwa usijiingize ndani ya mambo usiyoyajua ndewe wala sikio, nisamehe sana kwani sikukusudia" (uk.254)*

Katika hali hiyo Nana alilia sana hadi akamfanya Faisal aliye pia mwishowe walirejesha uhusiano na wakaingia gari kurudi nyumbani Faisal alikuwa amekuja pale kwenye msitu wa Ngezi kujituliza na kujikumbusha penzi lake na Bi. Mkubwa.

**Mwanamke kama mwanafalsafa**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Falsafa ni taaluma inayo dadisi hali halisi ya maisha ya binadamu kwa kuzingatia imani, mila, desturi, pamoja na mienendo aliyonayo binadamu katika jamii yake, huku akitafakari njia sahihi na bora za kuweza kutatua changamoto mbalimbali anazo kabiliana nazo katika maisha yake ya kila siku.Nana kutokana na busara na weledi wake aliweza kuibua falsafa ya vitu na mambo na aliyoyasema yakawa ya kweli.Kwa mfano, wakati kwake hukuwa wa jua kuchomoza na kutua au majogoo kuwika bali falsafa ya wakati ilikuwa kuenda na usasa.Usasa ambao mambo mengi yamechimbuka na yalihitaji maarifa na uelewa ili kupambana nayo.Nana anaibua falsafa yake kwa kusema hivi:

*"Hakika nyumba ni daraja ya mwanzo ya mafunzo ya binadamu yeyote yule-alihitimisha Nana-mafunzo ya wazazi na wana wao, ya ndugu na ndugu, ya uraia na uongozi wa aina yoyote. Yote huanza katika kiini cha baba na mama, kaka na dada-katika undani wa tabia za watu hawa, undani ambao hauduhushiwi sana siku hizi katika dunia inayojali pesa na utajiri wa dhuluma" (uk 160-161)*

Kwa mujibu wake Nana suala la maadili hufunzwa pale nyumbani. Mama na baba ndio huwa sehemu muhimu katika kufanikisha hili. Pia kaka na dada huchangia vilevile kwa hili kutimia ikizingatiwa namna dunia ilivyo yaani huzingatia sana pesa na utajiri ambao hupatikana kwa njia zisizo za haki kama vile kuwadhulumu wanajamii wengine.Kutokana na maisha aliyoishi Nana aliweza kutambua kuwa binadamu huwa na nafsi mbili zinazoshikana mikono. Anasema hivi:

*"Ya ndani ambayo Wajapanii huita honne nay a nje ambayo huiita tatemae. Ingawa hali ya nje ndiyo inayoonekana waziwazi, ya ndani ndiyo inayotawala kuifanya dunia yake mtu na dunia ya watu wengine iwe njema au mbaya" (uk.161)*

Hivyo basi ni muhimu mtu kupimwa kwa *honne ya* ndani na wala si hiyo ya nje kwani kupitia kwake ndio mtu hujijengea dunia yake n ahata pia kuathiri dunia ya watu wengine vilevile.

**Mwandishi alivyomsawiri mwanaume katika Riwaya ya Nyuso za Mwanamke kwa upande chanya.**

**Mwanaume kama mwenye kutoa maamuzi katika familia.**

Mwandishi amemsawiri mwanaume kuwa ndiye mwenye uwezo wa kutoa maamuzi mengi katika familia. Tuelezwa namna babayake Nana anavyomshurutisha kuolewa na Dusa japo Nana hakuwa tayari kwa jambo hilo. Anapojaribu kulipinga hili anapokea kijapo kwa kutoka kwa baba yake. Hili linadhihirishwa hivi:

*"Kwa nini? Kwa nini umenipiga baba?""Wewe sawasawa na mama`ako" Aliniambia.*

*Mimi sawasawa na mamangu? Ilinishitusha sana kauli hiyo. Mimi sawasawa na mamangu kwa vipi?" Kwa utukutu wangu labda? Kwa kuhalifu amri? Nilijiuliza hivyo kwa sababu mimi simjui mamangu. (uk.44)*

Jamii nyingi za Kiafrika uongozwa na mfumo wa ubabe –dume ambao humpa mamlaka mwanaume dhidi ya mwanamke hivi kwamba mwanaume huwa na uwezo wa kufanya maamuzi ambayo mwanamke ni sharti ayafwate.Wakati mwingine mwanamke anayeonekana kuenda kinyume na maamuzi haya katika jamii hii,hujipanda akiwa mpokezi ghadhabu kutoka kwa mwanamume.Ghadhabu hii ikijumuisha kichapo kwa mwanamke na hata

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt.Aggrey Wanyama, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.

kutawishwa.Baba yake Nana alikuwa na mpango wa kumuoza Nana kwa Dusa,ila Nana anakataa jambo hili linamkasirisha baba yake Nana ambaye anamchapa kofi.

Suala la kumweka mwanamume juu ya mwanamke halifai kwa sababu mwanamke ni kiumbe huru ambaye ana uwezo wa kujiamulia masuala muhimu ambayo yanaathiri maisha yake. Kulingana na Steady (1981), mwanamke wa Kiafrika ndiye anayefahamu hali yake na hivyo ana uwezo kupinga hali zinazomdhulumu. Nana analifahamu hili hivi kwamba anakataa kushurutishwa kuozwa kwa Dusa kijana mwenzake ambaye kulingan naye hakuwa amemchagua.

**Mwanaume kama mhusika anayefaa kustareheshwa.**

Mwandishi anamsawiri mwanaume kuwa mhusika anayefaa kustareheshwa katika jamii. Mara nyingi katika jamii za kiafrika pindi mwanamke anapoozwa na mahari kulipiwa, jukumu lake litakuwa basi kumshughulikia mumewe.Bi. Mkubwa anamfokea Nana kuwa anataka kuolewa ndio athibitiwe na mwanaume. Hili linaonyeshwa na mwandishi hivi:

*"…Unataka kuolewa, hujui kuolewa ni kudhibitiwa na mwanaume...? (uk.286)*

Ndoa huwa asasi muhimu katika kuendeleza jamii yoyote ile, ila katika ndoa hii wanawake hupitia madhila mengi sana. Kwanza huwa wamepoteza uhuru wao hivi kwamba wanathibitwa na mwanaume ambaye wanafaa kumfanyia kila kitu; kumfulia, kumlea watoto na hata pia kumstarehesha usiku.Bi. Mkubwa anamtahadharisha Nana dhidi ya kujiingiza katika asasi kwa sababu ana ufahamu kuwa, mwanamke akishaingia katika ndoa huwa basi kama mtumwa kwa mwanaume.

**Mwanaume kama mnyamavu.**

Msimulizi anatueleza kuwa Faisal rafikiye alikuwa mchache wa maneno wakati walipokuwa kwenye mazungumzo wakiabairi gari. Mwandishi anadokeza hivi:

*Tumo garini sasa.Siku zote tukiwa garini mimi ndiye nianzishaye mazungumzo. Hii ni kwa sababu Faisal ni mnyamavu. Hapendi kusema. Labda anachelea kujifitini. Hata nikimsemesha, kauli inayomtoka huwa ya mkatokato tu. Majibu yake ni mabutubutu. Ajabu lakini, leo alianzisha mazungumzo yeye. (uk.115)*

Faisal kutokana na hali aliyokuwa amekumbana nayo katika maisha ilimfanya kuwa mtu mtulivu hivi kwamba ilikuwa ni nadra kujihusisha katika mazungumzo yoyote yale

**Mwanaume kama mhusika mwenye maadili**

Kupitia kwa mhusika Amour hili linajitokeza. Ameonesha kuwa na maadili kutoka kwao Abudhabi kwanza tukizingatia kuwa alikuwa kijana mdogo ambaye angejiingiza katika anasa huku akifuja mali ya baba yake Bwana Faisal.Badala ya kutenda hili Amour anakuwa mtu mwenye maadili kwa kuwajibikia shughuli zake ipasavyo. Hivi kwamba Bi. Matuka alifurahishwa na utendakazi wake hivi kwamba anamrai kumtafuta mwanamke ili kumwoa na kuweza kukamilisha duara la maisha. Pia Amour na baba yake walipokaa kitako ndani ya mkahawa mmoja ili kujuliana hali Amour alimjuza babake kuwa alikuwa ameingia miaka mine hivi. Baba alimshangaa kwa kutojioneshana kwake muda huo wote. Amour anamweleza baba yake kuwa:

*…hakutaka kumtia hasira babake kwa kuingilia kati ya uhusiano wao, yeye Faisal baba mtu na binti anayeitwa Nana ambaye yeye babake husuhubiana naye kama chanda na pete, kila dakika na kila pahala. (uk.250)*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Kutokana na maadili haya ya Amour, Nana aliyekuwa mwingi wa nidhamu anamkubali na kupenda na kuamua kuishi naye kama mume na mke.

**Mwanaume kama mwajibikaji**

Kuwajibika ni ile hali ya kutekeleza wajibu uliopewa bila ya kushurutishwa wala kufutwa. Kupitia kwa mhusika Amour suala hili linabainika, baba yake Bwana Faisal alimwachia biashara na mali yake ili kuiendesha. Kwa upande wake Amour anajitolea kwa hali na mali kuendesha biashara hii hadi ikapanuka zaidi. Hakulaza damu wala kutelekeza wajibu huu muhimu. Mwandishi anadhihirisha hivi:

*…ile biashara inayopanuka bila kikomo ambayo yeye Amour aliilia kiapo kuiendeleza na kuikuza, ili kama angerudi babake, angekuta imetutumuliwa, imetanuliwa na kuongezwa kwa kiwango kikubwa nay eye kijana wake. Na si hayo tu, lakini babake angemkuta Amour amejaa ujuzi na uzoefu wa mwanabiashara mahiri. Amour kwa hivyo aliitekeleza dhamana yake vilivyo, mpaka akawa hana nafasi ya kutosha na maisha yake mwenyewe. (uk.268)*

Ni wazi kuwa suala la uwajibikaji kazini mara nyingi si rahisi kwa wengi wa wanajamii. Wengi wao huhitaji kufuatwafuatwa ili kuteleza lile wanalofaa kufanya. Jambo hili huwa si nzuri. Amour anajitokeza kuwa mhusika mwajibaki ambaye anaweza kuaminika na kuteleza majukumu yaliyo chini ya uangalizi wake pasi na kushurutishwa.

**Mwandishi alivyomsawiri mwanaume katika Riwaya ya Nyuso za Mwanamke kwa upande hasi.**

**Mwanaume kama mpenda vurugu**

Mwandisihi amemdhihirisha mwanaume kama mhusika anayeendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke katika jamii kwa kuendeleza vurugu dhidi yake. Nana anatueleza kuwa, pindi mama yake Bi. Mkubwa alipoolewa na Simai, alitambua kuwa mama yake ameolewa na mpenda –kupiga –wanawake. Anasema hivi:

*Baada ya muda mfupi tu wa kuolewa na Simai, Nana alitambua amekutana na mpenda –kupiga-wanawake. Mara leo Bimkubwa alipigwa kibao akavimba uso kwa sababu kachelewa kupika. Kesho alivimba mdomo kwa kibao alichozabwa nacho bila hisia wala huruma. Mara kesho kutwa alivunjwa mkono kwa dhoruba ya mwanamume huyo asiye na uonelevu wa aina yoyote. (uk.288)*

Ndoa imetukia kuwa mojawapo ya asasi inayomkandamiza mwanamke wa Kiafrika.Wanawake wengi wanaozwa na kujipata katika asasi hii huwa ni kama watumwa kwa mwanaume. Hawawezi kurejea kwao kwa sababu tayari washalipiwa mahari hivi kwamba hulazimika kuvumilia mateso yote kutoka kwa mwanamume huyu. Huku ni sawa na kuwa mtumwa.Bi. Mkubwa anajipata kuwa mpogezi wa kichapo kutoka kwa Simai ambaye aliolewa naye. Anampiga kila siku jambo kulingana na Nana linamkasirisha sana.

**Mwananume kama mpenda anasa**

Mwanaume amesawiriwa na mwandishi kama mhusika anayependa anasa na yupo tayari kutumia rasilmali yake kulitekeleza hili. Tunaelezwa na mwandishi hivi:

*Simai alivutiwa mara moja alipomwona Bimkubwa.Simai, mchuuzi wa samaki pale mnadani, moyo wake ulimshawishi na kumwambia lazima ampate mwanamke aliyeitwa Bimkubwa. Na*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

*haikuwa rahisi maana wanaume wote pale mnadani walitokwa roho na mwanamke huyo. Kwa hivyo alianza kummiminia mashazi kwa mashazi ya samaki wa bure yawe chambo cha kumnasa. (uk.288)*

Tamaduni za Kiafrika zimemdhalilisha mwanamke kiasi kwamba zinamlinganisha kama chombo cha starehe kwa mwanamume. Kwa kuwa mwanaume ana nguvu za kiuchumi ambazo hana mwanamke, hii umpa uwezo wa kuzitumia rasilmali zake hizi katika kuwatumia wanawake kujistarehesha. Simai anatumia uwezo wake wa kiuchumi kumnasa Bi. Mkubwa ili aweze kushiriki mapenzi naye.

**Mwanaume kama mwendelezaji wa dhuluma ya kingono dhidi ya mwanamke.**

Suala la kubagwa kwa mwanamke limekuwepo katika jamii nyingi za Kiafrika.Wafeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa mwanamke mara nyingi anadhulumiwa kimapenzi kwa sababu ya jinsia yake.

Tunaelezwa na mwandishi kuwa Fatuma alinajisiwa na mjomba wake akiwa mdogo na hata alipokuwa mkubwa. Hili linadhihirishwa hivi:

*"…Hakuna hata mmoja aliyethubutu kumkabili huyo mjomba…"*

*Hakusema hata neno moja hata kama alitukanwa na kupigwa makofi namna gani na Selemani Kijogoo.Kwa ufupi Bimkubwa alikuwa katiwa mfukoni mwa koti la Selemani Kijogoo na humo hakuchungulia nje wala kufurukuta. (uk.290-291)*

Vilevile tukio hili linamfanyikia Bimkubwa wakati anapoajiriwa na Mhindi dukani kuuza nguo, wanaposalia pekee yao mwendo wa jioni Mhindi huyo anambaka Bimkubwa, na kwa bahati mbaya Bimkubwa anapata mimba.

*Siku moja alipobaki na Bimkubwa peke yao walipokuwa wakifunga duka, alimkamata kwa nguvu na kumbaka Bimkubwa(uk.288)*

Mwanamke kwa mara nyingi ameendelea kunyanyaswa na jamii yake kwa sababu ya jinsia yake.Unyanyasaji wenyewe hukihusu sana suala la kingono.Wengi wao hunajisiwa na kutishiwa kutosema au kumwambia mtu mwingine.Fatuma ananajisiwa na mjomba wake ambaye katika hali ya kawaida katika jamii zinazozingatia usawa wa kijinsia anafaa kuwa mstari wa mbele katika kulinda maslahai yake.Vilevile Bi.Mkubwa anabakwa na mhindi mmoja ambaye alikuwa akifanya kazi kwake.Dhuluma dhidi ya mwanamke wa Kiafrika itaendelea endapo jamii haitajitokeza waziwazi kushutumu vitendo hivi na pia kuhakikisha kuwa kuna usawa wa kijinsia katika jamii.

**Mwanaume kama mwenye dharau**

Dharau ni tabia ya kupuunza, kutoheshimu na kumtweza mtu. Mwandishi amemchora mwanaume kama mhusika ambaye ana tabia ya kumdharau na kumdalalisha mwanamke. Hususan kupitia kwa vitendo vyake dhidi ya mwanamke. Mhusika Fatuma ananajisiwa na mjomba wake, anapopata mimba mjomba wake anamtishia asiseme. Wazee wa ukoo wake wanamsingizia kuwa alipata mimba hiyo mahali kwingine. Kwa kuwa jamii mara nyingi inamsikiliza mwanamume Fatuma anakatwa kauli kwa kutosikizwa. Anaeleza hivi:

*"…Hakuna hata mmoja aliyethubutu kumkabili huyo mjomba…" (uk.211)*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Matatizo mengi yanayomkumba mwanamke wa Kiafrika mara nyingi husababishwa na mwanamume ambaye amewekwa mbele na jamii yake.Huwa anasikiza hata kuaminika kwa kila jambo analosema hivi kwamba anapomtendea maovu mwanamke,jamii humpa fursa ya kujitetea huku mwanamke akipuuziliwa mbali.Fatuma anabakwa na mjomba wake ila wakati anapowaeleza wazee wa ukoo wake wanakataa kumsikiliza na kumshitumu kwa kumweleza kuwa alipata mimba hiyo mahali kwingine.Jambo hili ni la kuvunja moyo ikikumbukwa kuwa msababishi wa mimba hiyo alikuwa mjomba wake Fatuma.

**Mwanaume kama mtawishaji.**

Kutawishwa ni hali ya kuwafungia wanawake ndani ya nyumba kwa nia ya kutotakiwa watoke nje ili washirikiane na wanaume wasio wanaume zao na kuhakikisha kwamba wanawake wamewekewa mipaka. Utawa una asili yake katika dini ya Kiislamu na kama Momanyi (1998) anavyosema, huhusishwa na maandiko kutoka Kurani Takatifu.Nia ya kutawishwa wanawake ni kule kuwafungia kwa kuhofia kwamba wakichwa huru watatembea na kufanya mapenzi na wanaume wasio wao. Bwana Hila, ambaye ni babake Nana anaeleza kwamba Nana bado ni mwanagenzi wa dunia. Bwana Hila anashikilia kwamba lazima amhifadhi Nana hasa kwa vile bado ni msichana ambaye hajapata mume bado mdogo tu.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

**Hitimisho**

Utafiti huu umebaini kuwa waandishi huathiriwa na jinsia yao wanapowasawiri wahusika katika kazi zao za fasihi. Mwandishi wa kike anajaribu kuwainulia hadhi wahusika wa jinsia ya kike ikilinganishwa na mitazamo ya kihafidhina anayotumia mwandishi wa kiume katika kuwasawiri wahusika wa jinsia ya kike. Kwa mfano mwandishi Clara Momanyi amewasiri wahusika wa jinsi ya kike kwa njia chanya kwa kiwango kikubwa, amemtumia mhusika Mangwasha ambaye ni mwanamke amempa sifa nzuri na za kipekee. Yeye ni mlezi, mwajibikaji na ambaye anaonekana kuenda kinyume na mitazamo ya kihafidhina kumhusu mwanamke wa Kiafrika kwa kudhiriki kutenda sawa na mwanaume. Yupo kipaumbele kuhakikisha kuna amani baina ya Wakule na Waketwa katika jamii yake. Jambo ambalo kwa mara nyingi limekuwa likiachiwa wanaume katika jamii. Pale nyumbani kwake vilevile anajitwika jukumu la kukidhi mahitaji ya familia yake. Hii ni baada ya mume wake Mrima kujiingiza katika suala la ulevi na kutelekeza wajibu wake kama baba kwa watoto wake na mkewe Mangwasha.Momanyi pia amedhihirisha kuwa ukombozi wa mwanamke unakumbwa na changamoto si haba hususani kutokana na tamaduni potovu ambazo zinamweka mwanamke kuwa chini ya mwanaume. Wananyimwa fursa ya kutoa mchango wa kimawazo ili kuboresha jamii zao. Licha ya Mangwasha kufahamu kwa kina kiini cha kutoelewana baina ya Waketwa na Wakule kwa sababu alikuwa akifanya kazi katika ofisi ya Chifu Mshabaha ambamo masuala mengi yalijadiliwa mengi yakiwa na ruwaza ya kuwadhulumu Waketwa, hana fursa ya kumweleza Lonare kiongozi wao kwa sababu jamii yake haitambui mwanamke katika suala la uongozi.Vilevile Momanyi amedhihirisha jinsi juhudi za kumwinulia hadhi mwanamke huwa zinapingwa na wanawake wenyewe kwa kumtumia mhusika Sihaba ambaye anawatumia wasichana wadogo katika biashara haramu ya ngono badala ya kuwa mstari wa mbele katika kupinga masuala kama haya.Pia mhusika huyu anatumiwa na Sagilu ili kusambaratisha arusi kati ya Mangwasha na Mrima.Kwa upande wa kuwasawiri wahusika wa jinsia ya kiume na mwandishi wa kike ni kama kulipiza kisasi, yaani wahusika hawa wametweza katika hali zozote zile kupitia mtazamo hasi wa mwandishi dhidi yao. Kwa mfano, wamechorwa kama walevi, wavunja familia, katili, wapenda mali, washerati na hata pia wapinga mabadiliko katika jamii. Lengo hili la mwandishi ni kuwaasa wahusika hawa wabadilike na kuwa na matendo mema na mazuri. Momanyi amewasiriwa kwa uyakinifu wake jinsi wanavyowadhulumu wanajamii wengine. Kwa mfano kiongozi kama Sagilu anatumia uongozi wake isivyofaa anaagiza maziwa ambayo yametiwa kemikali nyingi ili yaweze kudumu, pindi watoto wanapoyatumia wengi wao wanaaga dunia. Mhusika huyu pia anawaangamiza wale wanaoshindana naye katika biashara. Vilevile mhusika huyu anasawiriwa kama mpinga mabadiliko katika jamii yake ambayo imekumbwa na uongozi mbaya. Wanajamii kama vile Lonare wanaojaribu kuleta mabadiliko wanakumbana na vikwazo si haba kutoka kwa wanajamii kama Sagilu.Mwandishi pia ameonyesha jinsi mhusika wa jinsia ya kiume anavyochangia kuvunjika kwa familia kwa sababu ya ukware wake usiothibitika.Sagilu licha ya kufahamu kuwa mwanawe Mashauri alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Cheiya bado anamshawishi kuwa mpenzi wake hadi wanapofumaniwa

wakitoka katika mkahawa mmoja na Mashauri,jambo linalomuuma sana Mashauri hadi kufikia uamuzi wa kutomwita wala kumtazama Sagilu kama baba yake hivi kwamba familia hiyo inasambaratika hivyo.

Said Muhamed kwa upande wake ameonekana akimkweza mhusika wa jinsia ya kiume. Kwa mfano amemdhihirisha kama kiongozi wa familia, tajiri na mwenye kupenda makuu na hata kama mwenye kutoa maamuzi. Kupitia mhusika Bw. Hila baba yake Nana hili linadhihirika amechorwa kama mhusika anayefaa kusikilizwa wakati anatoa maamuzi kuhusu suala fulani. Tunaona namna anavyopanga Nana kuolewa na Dusa, wakati Nana anapokataa anatawishwa na bwana huyu. Vilevile kupitia kwa mhusika Faisal tunaona namna mwanaume alivyo na uwezo na nguvu za kiuchumi kumshinda mwanamke.

Faisal alikuwa ni tajiri wa kupigiwa mfano alimiliki utajiri mkubwa ambao ulikuwa ukiangaliwa na mwanawe Amour.Kwa upande wa kuwasawiri wahusika wa jinsia ya kike ,mwandishi huyu amewadunisha wahusika hawa kwa kuwachora kama wasio na uwezo wa kujifanyia maamuzi yaani wapo chini ya mwanaume nyakati zote.Kwa mfano Bi.Mkubwa analazimishwa kuolewa na Bw.Hila pasi na kutaka jambo ambalo baadaye linamfanya kukimbia ndoa yake.Yaani wazazi wengi hawawapi wanawake fursa kuchagua wapenzi wao.Pia Nana anashurutishwa kuolewa na Dusa na baba yake.Mwandishi pia amemchora mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume kimapenzi.Tunaona namna Bi.Mkubwa anavyobakwa na mhindi ambaye alikuwa akifanya kazi huko.Mhusika mwanamke ametambulishwa kama mpogezi wa kichapo kwa kutaka kuenda kinyume na matakwa ya mwanaume ambaye jamii inamuona kama kiumbe cha hadhi kumliko mwanamke.Nana anachapwa kofi na baba yake kwa kukataa kuolewa na Dusa nahata jumba lake linateketezwa moto na Ngware aliyetumwa na Bw.Hila kwa sababu ya Nana kuamua kuolewa na Amour jambo ambalo Bw.Hila hakulitaka.

Kwa jumla waandishi wote wamedhihirisha kuwa bado kuna dhuluma dhidi ya mwanamke katika jamii licha ya mpito wa kiwakati na dhuluma hizi zinaendeshwa kupitia asasi za ndoa na tamaduni potovu.Kwa mfano suala la kumuoza mwanamke pasi na kuzingatia hisia zake.Mwanamke kutumiwa kama chombo cha starehe kwa mwanamume.Tunaoneshwa namna Simai alivyomdondokea Bi.Mkubwa alivyomwona mara ya kwanza na kuapa kuwa angeshiriki mapenzi naye.Vilevile Sagilu anatumia njia zote kumpata Mangwasha na kushiriki naye mapenzi jambo ambalo hakufaulu kwa sababu ya mtazamo wake Mangwasha kulihusu hili.Waandishi wote vilevile wameonyesha kuwa mwanamke ana uwezo wa kujikombolea hadhi na kuweza kupata uhuru wao.Nana anakataa kuozwa kwa Dusa ambaye alichaguliwa na baba yake n ahata kukimbia kwao kuenda kujitafutia maisha.Na baadaye anaweza kuolewa na Amour mwanaume aliyempenda yeye Nana.

## Marejeleo

Chesaina, C. (1987). Women in African Drama.Tasnifu ya PhD.Chuo Kikuu Cha Leeds.

De Beavour, S. (1949). The Second Sex.London: Pan Books Publisher.

Engels, F. (1975). The Origin of the Family Private Property and the State.New York: Pathfinders Press Inc.

Figes, E. (1978). PatriarchalAttitudes.London: Virago Press.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Dkt.Aggrey Wanyama, **
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Athari ya Jinsiaya Mtunzi katika Usawiri wa Wahusika katikaRiwaya zaKiswahili:Mifano kutokana na Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi.*

Lugano, R.S. (1989). Mwanamke katika Riwaya ya Kezilahabi: Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mavisi, R. (2007). Usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Z. Burhani.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Momanyi, C (2021). Nguu za Jadi.Nairobi: Queenex Publsihers Limited.

Millet, K. (1969). Sexual Politics.London: Virago press.

Said, A.M. (2010). *Nyuso za Mwanamke*.Nairobi. Longhorn publishers.

Steady, F.C. (1981). Black Women Cross Culturally.Cambridge: Mass Scherkman Publishing Co.Inc.

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2002). Uhakiki wa Fasihi: Nairobi.Phoenix Publisher.